KIVULINI MWA YESU

KIVULINI MWA YESU

MSAADA WA KIIMANI KWA WAKRISTO WANAOISHI NA VVU

JOAN YORBA-GRAY

Mungu Amedhamiria Ushindi (He Intends Victory)
1 -800-HW- HOPE
www.heintendsvictory.com

Kwa asili ya kitabu hiki, rejea za Biblia zimenukuliwa toka katika Biblia ziitwazo *Life Application Bible, New International Version,* hatimiliki 1988, 1989, 1990 na 1991 zilizotolewa na Wachapaji wa Tyndale House Publishers Inc., Wheaton, Illinois na Zondervan Publishing House, Grand Rapids, Michigan na toka katika Biblia iitwayo *The Thompson Chain Reference Bible, King James Version, Fourth Improved Edition*, copyright 1964, B.B. Kirkbridge Bible Co., Inc., Indianapolis, Indiana. *Webster's New Universal Unabridged Dictionary,* NY Barnes & Noble, 1996
Nukuu za Biblia katika tafsiri hii ya Kiswahili zinatoka katika Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa – Kenya [Nairobi] na Tanzania [Dodoma]

Kimehaririwa na Judy Odeli na Carol Skinner

Vielelezo vimetolewa na Glen F. Gray

Kimebuniwa na Richard Tinker

Picha ya Kwenye Jalada na © iStockphoto.com/José Luis Gutiérrez

Kimetafsriwa kwa Kiswahili na Frank Luvanda

KIVULINI MWA YESU
Hatimiliki 2001 na Mungu Amedhamiria Ushindi (He Intends Victory)
Chapisho la Pili 2004
Chapisho la Tatu 2006
Chapisho la Nne 2011

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa nakala, kudurufu, kuhifadhiwa katika mifumo ya kielektroniki pasipo ridhaa ya maandishi toka kwa mchapaji

Kimechapishwa Nchini Marekani

SHUKRANI

Shukrani kwa huduma ya MUNGU AMEDHAMIRIA USHINDI (HE INTENDS VICTORY) kwa kuuonyesha upendo wa Kristo kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Shukrani kwa Paul Allen, ambaye maneno yake ya kufaa, yalikuwa ni kama machungwa ya dhahabu katika vyano vya fedha (Mithali 25:11).

Shukrani kwa wapendwa wana familia yangu ambao waliniunga mkono na kunisaidia wakati nilipokuwa nikiumwa na wakati nilipokuwa na afya nzuri: shukrani kwa watoto wangu Daniel na Sevanne ambao walinifanya nione sababu ya kuishi hasa wakati nilipotaka kukata tamaa, shukrani kwa mume wangu Galen, ambaye upendo wake kwangu una nguvu kuliko VVU.

Shukrani kwa Mchungaji wangu Don Baldwin na mke wake Judy ambao waliipenda familia yangu pasipo masharti yoyote yale.

KWA HESHIMA YA

Chapisho hili la Kivulini Mwa Yesu linatolewa kwa heshima na kwa kumbukumbu ya mtoto wetu mpendwa Kurtis Edward Gray; ambaye alizaliwa tarehe 29 Machi 1982 na kufariki tarehe 22 Aprili 2010. Kurtis alikuwa akihuduma katika Jeshi la Marekani kwa miaka sita, ikijumuisha miezi 15 akiwa nchini Iraki. Vitisho vya vita na matatizo ya kifikra yatokanayo na mashambulio ya vita, pamoja na majeraha aliyoyapata wakati akipigana vita huko Ramadi, kwa pamoja vilisababisha mkanganyiko wa kimatibabu na kusababisha kifo chake kwa bahati mbaya. Lakini kutokana na kifo huja uzima. Na ndio maana kutokana na moyo wake uliokuwa na huruma kumetokea baraka ya kuweza kutoa chapisho hili.

Kurtis alikua akiwa shaidi wa maisha ya Joan, na alitambua vizuri baraka ya ukombozi—wa maisha iliyokuwa imenyakuliwa na shambulizi la UKIMWI. Kurtis alikuwa ni rafiki mwenye msaada kwa askari mwenzake aliyekuwa akiteseka kimyakimya kutokana na VVU katika mazingira ambayo alipaswa kuwa kimya. Ninafahamu kuwa mwanangu atafurahishwa kwa kuwa Kivulini Mwa Yesu kitatoa mwongozo kwa watu wengi watakaousoma ujumbe huu wenye nguvu na kuweza kumfikia Mungu, na kuweza kuishi tena kwa amani, na kuwa sehemu ya jumuia yenye upendo.

Kwa sasa Kurtis yupo salama katika kivuli cha Mungu Mwenyezi ambapo jua kali la Iraki haliwezi kuiunguza nafsi yake, na yupo mahali ambapo mwili na roho iliyoumizwa na vita inaweza kupata amani huku akiwa amekumbatiwa na Baba Mungu.

Image of Kurtis Edward Gray

Kurtis Edward Gray

YALIYOMO

Dibaji 11

Utangulizi 17

1. Wimbi Kubwa 25
2. Zaburi Ya 91 31
3. Kumkasirikia Mungu 37
4. Ugumu wa Kusamehe 43
5. Kwa Nini Iwe ni Mimi? 49
6. Kuitupa Tabia ya Hofu 55
7. Aibu 61
8. Dhamiri Mbaya 65
9. Zaburi Ya 119 na Mateso 71
10. Jaribu la Kujinyonga 77
11. Msamaha Warejewa 83
12. Mambo ya Upendo Hapo Zamani 91
13. Zaburi Ya 118 99
14. Mtandao wa Dunia Nzima 105
15. Ugonjwa wa Lazaro 109
16. Zawadi Yangu 115
17. Maneno ya Ziada 119

DIBAJI

“Bwana, kwa nini ulinikutanisha na mwanamke huyu katika maisha yangu wakati ambapo siwezi kumwoa?” Hivi ndivyo nilivyolia hali nikiwa nimechanganyikiwa baada ya kuwa nimefahamiana na Joan kwa takribani miezi sita, huku nikiwa nimetambua kuwa anaishi na VVU, na wakati huo huo nilikuwa nikimpenda sana kisirisiri. Kwa nyongeza tu, nilikuwa nimeiweka picha yake katika kabati mojawapo ofisini kwangu ili kumkumbusha Mungu kuwa haikuwa vizuri kwa yeye Mungu kunitania namna hiyo. Je, hii ilikuwa ni aina fulani ya mahangaiko ya kimungu au ilikuwa ni kupata adhabu kwa ajili ya kosa la mtu mwingine—nilikuwa nikijiuliza ni kwa nini Mungu alikuwa akikizuia kitu chema kisiwe changu? Kwa kweli sikuwa kama Maria ambaye katika wimbo mmoja aliimba wimbo wa kutakiana mapenzi mema, “Mahali fulani katika ujana wangu au katika utoto wangu nitakuwa nilifanya kitu fulani kizuri.”

Nilikutana na Joan majira ya kiangazi mwaka 1989 katika shughuli ya kijamii ya Kanisa. Joan alikuwa ni “mjane anayeishi na UKIMWI” akiwa na watoto wadogo wawili, wakati huo mimi nilikuwa ni baba mgane mwenye watoto watatu. Hivyo, niliona wazi kuwa sisi wawili tungeweza kuwa na familia nzuri ya watoto watano inayofanana na ngazi nzuri—na huo ndio ukweli ulioukuwa unatisha zaidi kuliko VVU! Wakati huu ilikuwa ni mwanzoni mwa miaka ya tisini na tisa na wakati huo taarifa za msingi na kutosha juu ya namna ya kujilinda na maambukizi ya VVU. Hivyo, pamoja na ukweli uliokuwa umefichika kati yetu, yaani ukweli wa kuwa tunapendana, ililazimu kujiweka kando na suala lolote la kimapenzi. Pamoja na hayo, tukawa marafiki wa kweli na wa karibu kwa kuwa tulikuwa tuna malengo na mitazamo inayofanana. Kimsingi, uhusiano wetu ulikuwa mzuri kwa kuwa sisi sote tulihitaji nafasi ya kuomboleza ili kupata

faraja kutokana na wapendwa wetu tuliowapoteza: Joana alikuwa amempoteza mumewe kutokana na UKIMWI na kisha akagundulika kuwa na maambukizi ya VVU, kwa upande wangu nilikuwa nimekabiliana na talaka isiyotarajiwa ambayo iliivunjavunja familia yangu, huduma yangu, kazi yangu, pamoja na heshima yangu binafsi. Kwa kweli ni lazima nikiri kuwa maombi, uponyaji, na huduma yenye hekima ya Mchungaji Don Baldwin ilitufanya tupate mtazamo mpya kwa uhusiano wetu ambao ulikuwa bado haujakamilika katika ngazi ya ndoa.

Hapo kabla nilikuwa nimewasiliana na wanawake wengine, lakini niliona kama ninafanyiwa hila. Hivyo nilipoanza kutambua jinsi ninavyompenda Joan, na jinsi anavyofaa kuwa mwenzangu wa nafsi yangu, basi hatimaye “nikapata wazo” na nikaamua kutafuta maelezo zaidi. Nilikuwa nimeshafikia wakati wa kufanya maamuzi, na hivyo nilihitaji kupata uhakika juu ya hatari na nidhamu inayohitajika ili kufanya “mapenzi-salama” na jinsi tunavyoweza kuziunganisha familia zetu.

Uchaguzi ulikuwa wazi kabisa: ni kuomba uwezekano wa kuwa mwanandoa wa Joan au kuachana kabisa na suala la kuifuatilia nafsi nzuri ya Joan ili awe mwanandoa wangu. Asubuhi moja, uhalisia mzito ulijitokeza ulioonyesha kuwa ninampenda sana Joan kuliko hofu ya VVU, na nikaona kwamba kama Mungu angelimpatia Joan miaka miwili ya kuishi, basi ni heri nitumie hiyo miaka miwili kwa kuishi na Joan kuliko kuishi miaka ishirini pasipo kuwa naye.

Kwa kweli fikra na hisia zangu kuhusiana na Joan zilikuwa sahihi. Nilipomfahamu Joan kwa mara ya kwanza alikuwa akiwalea watoto wake kwa umakini mkubwa huku akizingatia miiko na desturi za Kikristo, lakini ukweli ni kuwa alikuwa na kila sababu ya kuwa na machungu kutokana na magumu aliyokuwa akiyapitia. Pia alikuwa akifanya kazi kama mhudumu wa jamii wa Kikristo na mshauri hadi alipolazwa kutokana na kuugua. Katika ulimwengu wa wachukuaji na watumiaji, Joan ni

mtoaji—yeye hajioni kuwa ni mtu anayestahili kuonewa huruma na kufanyiwa hisani, bali anajiona kuwa ni mdaiwa anayestahili kuwashirikisha wengine upendo wa Mungu kutoka katika maisha yake yaliyojeruhiwa. Joan alikuwa wa kwanza kukiri kushindwa kwake na kukiri matatizo katika mchakato wa kuelekea afya ya kihisia na kiroho. Yeye si mtu aliyejengeka kwa usiku mmoja na wala si yule aliyefanywa kuwa mtakatifu. Ni kwa kupitia kazi ngumu na machozi ndivyo vilivyomfanya awe na mkono wenye kutoa na mwenye moyo ambao hauja haribiwa na ubinafsi, na wala hajairuhusu nafsi yake kutetemeka wakati alipokutana na magumu ya kusamehe, na wakati alipokutana na vijana wadogo wenye kutia uchungu, na watu wenye tabia ya kuwahukumu watu wengine. Na jambo bora kabisa ni kwamba Joan alinikubalia ili niweze kumpenda na yeye aweze kunipenda.

Tangu tulipofunga ndoa yetu mwaka 1994, kwa kweli tumepata kukua kwa namna mbalimbali ambazo hatukuzitarajia, na hali hiyo imetufanya tuweze kuyashinda masumbufu ya maisha na kuipata raha ya upendo. Tumegundua kwamba sio tu kwamba Mungu amedhamiria ushindi, bali pia anaongea kupitia Neno la Kristo katika maisha yetu binafsi. Kwa namna ambavyo Mungu ameyasamehe makosa yetu ya zamani, na jinsi anavyoendelea kutukomboa toka katika bahati mbaya, kwa kweli tumepata kimbilio katika siri ya upendo wake. Joan haishi chini ya VVU wala chini ya wingu lake zito, bali anaishi chini ya kivuli cha Mungu chenye ulinzi tosha. Hali nikiwa na “Joan wangu” karibu nami tunasonga mbele kwa ujasiri hali tukiiona siku ya kesho yenye matumaini—wakati huohuo tumaini la Kristo la kuhudumu linatuita kuhudumu kwa upendo jambo ambalo ni kubwa kuliko mkanganyiko na kuliko kupoteza.

Galen Beckwith Yorba-Gray

UTANGULIZI

Nilizaliwa na kukulia California nikiwa na asili ya wahamiaji wa Kihispania waliohamia California wakiwa na wachunguzi wa kale, pia ukoo wangu umechanganyikana na asili za Kifaransa, Kidachi, na Kijerumani. Familia yetu ilikuwa ya Kikatoliki na tulikuwa ni watu tuliokuwa tukienda kanisani mara kwa mara hadi wakati ambapo wazazi wangu walipotalikiana nikiwa na umri wa miaka 14. Nilipokuwa mtoto nilimpenda Mungu na nilizifahamu hadithi nyingi za Biblia na za watakatifu, na nilizipenda ana. Hata hivyo, baada ya wazazi wangu kutalikiana, nilijikuta nikiwa kijana mdogo aliye peke yake na mwenye msongo wa mawazo, na nikageuka na kuiacha imani yangu. Lakini, ninapogeuka na kuyaangalia maisha yangu ya zamani, ninatambua kwamba Mungu alikuwa akiilea mbegu ya kiimani iliyokuwa imependwa katika maisha yangu nilipokuwa bado mtoto hata katika kipindi kile nilipokuwa nimeasi.

Nilikutana na mume wangu wa kwanza Ray tukiwa chuoni na nilivutiwa sana na upendo wake, na moyo wake mwepesi usio na uzito. Ray alikuwa na umri mkubwa maana alikuwa amehitimu katika masomo ya shule ya juu, na alikuwa amefanya kazi kwa miaka kadhaa kabla ya kurudi tena chuoni kwa masomo. Kwa kweli niliifurahia hali yake ya kuwa na ujasiri na jinsi alivyokuwa na stadi mbalimbali hasa ukizingatia kuwa mimi nilikuwa sijawahi kuishi peke yangu, nilifurahia kuona jinsi alivyoweza kuishi kwa kujitegemea. Mimi na Ray tulikuwa na matakwa na malengo yaliyokuwa yakifanana sana na ilipofika mwaka 1976 tulifunga ndoa. Ndoa yetu ilikuwa ni nzuri sana kwa namna mbalimbali lakini kuna nyakati nyingi ambapo alionyesha hali ya kukata tamaa, kutokuwa na amani, na alionyesha kuwa na msongo wa mawazo na kutoridhika. Tulipata ushauri mbalimbali

lakini bado alionekana kuzidi kuwa na huzuni na mwenye hasira na asiye na furaha kabisa. Wakati huo tulikuwa na watoto wazuri wawili, mtoto mzuri wa kiume aliyeitwa Danieli aliyezaliwa mwaka 1980 na binti mrembo aliyeitwa Sevanne aliyezaliwa mwaka 1982, na kwa kweli tulikuwa na maisha mazuri sana ya kifamilia. Niliamini kwamba ndoa zote zinakabiliana na milima na mabonde na kwamba kipindi tulichokuwa tukikipitia kilikuwa ni sehemu ya majaribu ya kawaida ya maisha ya ndoa.

Mwaka 1986 alipokaribia kusherehekea sikukuu yake ya kuzaliwa ya mwaka wake wa 40 Ray alizidi kujitenga na kutokuwa na mawasiliano. Raye aliendelea kuwa na msongo mzito wa mawazo kiasi kuwa nikadhani anakabiliana na tatizo la msongo wa mawazo wa maisha ya kati. Aliendelea kuipenda kazi yake, na aliendelea kuipenda familia na maisha ya nyumbani lakini kuliendelea kuwa na ufa mkubwa wa kimawasiliano kati yetu. Ushauri ambao tulijaribu kuupata haukuweza kutusaidia kuvunja kuta zilizozuia mawasiliano kati yetu. Wakati huo, kama miaka mitano iliyopita nilikuwa nimerejea Kanisani na nilikuwa nimeyatoa maisha yangu kumfuata Yesu. Kipindi hicho niliona jinsi nilivyozidi kupata nguvu hasa pale nilipozidi kukua kiroho, lakini imani yangu ilionekana kujenga umbali zaidi kati yangu na Ray. Ray aliiona imani yangu na jinsi nilivyokuwa na ujasiri kwa Mungu kuwa ni tishio kwake. Ray alitaka niache kwenda Kanisani nilipokuwa nikisali lakini mimi nilikataa kukatisha uhusiano wangu na Bwana. Hatimaye nilitambua kwamba kwa kuwa aliona ni kama “nimemsaliti” kwa mimi kujitoa maisha yangu kwa Kristo, basi aliamua kunisaliti kimapenzi. Akili za mwanadamu zina uwezo mkubwa wa kuhalalisha jambo ambalo mtu anataka kulifanya.

Ray hakuwa mtu wa kupenda kujirusha na kwa sababu hiyo sikuwahi kufikiria kwamba ana mahusiano mengine ya kimapenzi nje ya ndoa. Kwa kweli alikuwa ni mtu wa kukaa sana nyumbani. Alisafiri mara chache kikazi lakini alipokuwa hana safari za kikazi aliutumia

muda wote akiwa nyumbani. Ray alikuwa akiendesha baiskeli yake siku za mapumziko, na alikuwa akifanya kazi za usafi katika uwanja wetu, na alishiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na hasa kwa familia yetu iliyokuwa pana. Kwa kweli Ray alikuwa ni fumbo kwangu.

Mwaka 1987 afya yake ilianza kuzorota na alikuwa akikabiliana na maumivu ya kooni, na akawa na maambukizi na matatizo katika mfumo wa upumuaji. Siku moja mwezi Februari mwaka 1988 aliugua sana kiasi kwamba hakuweza kupumua na hivyo kushindwa kutembea hata kwa zaidi ya hatua tano pasipo kupumzika. Usiku wa siku hiyo Ray alilazwa. Baada ya kupata vipimo vingi kwa siku nyingi alizokaa hospitalini, hapo ndipo tulipopokea pigo la kukatisha tamaa, hii ni kwa sababu Ray alionekana kuwa na ugonjwa ujulikanao kitalaamu kama *pneumocystis carinii pneumonia*, ambao ni ugonjwa unaohusianishwa na UKIMWI. Yaani kwa kifupi alikuwa na UKIMWI!

Ninakumbuka nilipoambiwa kwamba ana UKIMWI niliona ni kama nimepigwa na nyundo nzito. Nilipata mshtuko mkubwa, niliumia na nikajawa na hasira. Mwishowe nilitambua kwamba Ray alikuwa amenisaliti, na hivyo fumbo nililokuwa nikiliona kwa Ray lilianza kuwa wazi kwangu. Yaani kuhusu ule umbali aliokuwa nao kwangu, vile vikwazo vilivyokuwepo kati yetu, na matatizo ya maisha ya umri wa kati vyote hivyo vilidhihirisha jinsi alivyokuwa amenisaliti kimapenzi, jambo ambalo hatimaye alikuja kulikiri bayana. Alikuwa akiishi maisha ya kudanganya. Usiku huo nilirudi nyumbani huku nikijiandaa kuachana naye na kuondoka ili nimwache peke yake.

Nilipokuwa nyumbani na nilipokwenda kulala kitandani nilijawa na hofu. Ray alikuwa ametusaliti; ni lazima niondoke nimwache. Nilichukizwa sana, familia yetu ilikuwa imepata mpasuko, maisha ya watoto wetu yalikuwa yamevunjwa vunjwa, na nilikuwa na hofu kuwa hata mimi hapo baadaye nitaonyesha dalili za UKIMWI.

Kwa kweli nilipata utisho ambao sijawahi kuupata maishani.

Kadri nilivyokua nikipambana na mawimbi ya kutisha ya kihisia, simu iliita. Aliyepiga simu alikuwa ni Ray. Ray alikuwa na hofu sana na alitambua kwamba alikuwa amekikaribia kifo. Nilitamani sana kwamba angelifanya mapatano ya amani na Mungu wakati atakapokuwa karibu na kifo kutokana na ugonjwa huu wa kutisha. Ray aliniomba msamaha kwa tendo lake la kuisaliti ndoa yetu na kwamba alitaka kuyaweka mambo sawa. Ray alitaka kubadilika na kuyakabidhi maisha yake kwa Mungu. Nilimwongoza sala ya kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wake, alitubu dhambi zake zote alizokuwa amezitenda na akaahidi kubadilika. Tuliongea sana usiku ule kuhusiana na usaliti wake na alieleza wazi kuwa alitaka kubadilika. Kwa upande wangu hali hiyo niliilinganisha na habari ya Yona na watu wa Ninawi. Yona alitaka Mungu awahukumu watu wa Ninawi mara moja, lakini Mungu alikuwa na mpango tofauti. Kwa upande mmoja Yona alitaka kumtii Mungu, lakini kwa upande mwingine Yona alitaka hasira ya Mungu iwashukie wenye dhambi. Nilijisikia kuwa na nguvu, lakini wakati huo huo nilikuwa na mawazo yaliyokanganyika, nilikua na hasira na nilijawa na chuki na wakati huo huo nilikuwa na furaha kwa tendo la moyo wa Ray kubadilika kiimani.

Kutokana na toba yake nilipata matumaini kwamba ndoa yetu itapata matengenezo na hii ni kutokana na ukweli kuwa mimi nilipokutana na Kristo maisha yangu yalibadilika moja kwa moja. Kwa bahati mbaya hali haikuwa hivyo kwa upande wa Ray.

Baada ya usiku huo tulipozungumza, Ray hakuendelea kuwa wazi. Ilikuwa ni kama mlango uliokuwa umefunguka ulijifunga kwa kubamizwa. Hakunieleza kikamilifu kuhusu mahusiano yake ya kimapenzi nje ya ndoa na wala hakuonyesha nia ya kutibu majeraha aliyokuwa ameyafanya kwa watoto na kwangu mimi.

Kwa kweli siwezi kuuhukumu moyo wa Ray. Sina hakika kama alitubu kwa kweli lakini nilikuwa nikiona

aibu sana kutokana na tabia yake, na pia sikuwa na ujasiri wa kuweza kulisema hilo mbele za Mungu, wakati mwingine nilifikiri kwamba alifanya toba ilimradi tu nisiondoke na kumwacha peke yake. Ni Mungu tu ndiye anayeujua moyo wake. Hata hivyo, Ray aliendelea kuwa mbali nami na kwa watoto wetu. Alianza kuugua ugonjwa wa kiakili unaoambatana na UKIMWI, ugonjwa ambao pia uliathiri uwezo wake wa kufikiri na hivyo kuathiri mawasiliano ya wazi kati yetu. Kutokana na matokeo ya ugonjwa huo ndoa yetu haikuweza tena kuponywa na hivyo ikavunjika. Hata hivyo, niliamua kukaa naye na tukawa tunaishi kama majirani tunaotumia nyumba moja, na si kama mume na mke. Sababu moja iliyonifanya nibaki naye ni kwamba alikuwa mgonjwa sana na isingekuwa sahihi kumwacha wakati akiwa mgonjwa mahututi kutokana na tabia yake iliyomfanya apate ugonjwa huo. Nilitambua kwamba alihitaji kutunzwa na niliamini kwamba huo ulikuwa ni wajibu wangu. Kwa nyongeza, niliona kuwa haitakuwa na mana kuongeza madhara ya talaka huku nikijua kuwa atafariki. Kwa kweli niliona itakuwa ni kuwafanya watoto wapate shida mara mbili ya kumpoteza baba yao, yaani kwa talaka na baadaye kwa kifo. Niliona kwamba kwa wakati huo tulikuwa na machungu mengi ya kukabiliana nayo na kwamba haikuwa busara kuongeza machungu mengine.

Katika majira ya kiangazi ya mwaka 1988, nilichukua uamuzi wa kijasiri wa kwenda kupima kipimo cha VVU na matokeo yalionyesha kwamba nilikuwa nimeambukizwa na VVU. Kwa mara nyingine tena, nilikabiliana na siku za kukosa usingizi na zilizojaa hofu. Nilijiuliza maswali mengi, kwamba nitawezaje kufanya mambo yote pamoja—yaani kumtunza Ray, kufanya kazi, kuwatunza watoto wangu, na kuitunza afya yangu pia? Kwa kweli ilionekana kuwa ni jambo lisilowezekana. Nilihofia kwamba watoto wangu wangeliweza kuwa yatima. Nilijisikia huzuni na maumivu makubwa kutokana jinsi maisha yangu yalivyokuwa yameshambuliwa. Nilipambana sana na hali ya kifo ndani yangu. Nilijiuliza nitaishi kwa

muda gani? Wakati huo kulikuwa na dawa chache sana za kupunguza makali ya VVU na dawa hizo hazikuweza kupunguza ukuaji na ongezeko la idadi ya VVU mwilini. Hivyo kwa wakati huo kugundulika kuwa una maambukizi ya VVU ilikuwa ni sawa na kupewa hukumu ya kifo.

Kipindi hicho kilikuwa ni kipindi chenye upweke sana katika maisha yangu. Ray alikuwa akijijali yeye mwenyewe, ndugu wengi wa familia zetu walipata mshtuko na hivyo wakaamua kujiweka mbali nasi, na kutokana na aibu na unyanyapaa uliokuwa ukiandamana na VVU sikuweza kuwaeleza watu wengi kuhusu hali yetu hiyo. Nilikuwa ni Mkristo, niliyekuwa katika ndoa, mwanamke mwenye mahusiano ya kawaida ya kindoa na sikuwa nikitumia madawa ya kulevya. Kwa kweli wakati huo hakukuwa na watu wengi waliokuwa kama mimi. Watu wengi walioifahamu siri ya familia yetu walikuwa hawapendi kuja nyumbani kwetu kwa kuwa walikuwa wakiuhofia UKIMWI, mateso yake na kifo.

Kuna nyakati nyingi ambapo Bwana alikutana nami katika hizo siku za giza na upweke. Ni nyakati ambazo Bwana alinifariji na kunionyesha upendo. Bwana alinipatia nguvu na ujasiri. Ninaufikiria usiku mmoja ambapo nilikuwa na hofu sana huku nikijisikia kuchanganyikiwa, wakati huo nilikuwa nikiomba kwa nguvu sana ili kupata ukombozi. Ghafla nilipata faraja ya kutosha kama vile ninafunikwa blanketi wakati wa baridi, hali hiyo ilinitokea ikianzia kichwani hadi miguuni. Hilo blanketi la kiroho toka kwa Bwana lilinipatia utulivu mkuu ambao uliondoa hofu na mashaka yangu yote. Ninakumbuka jinsi nilivyokuwa nimejizamisha ndani ya hiyo faraja toka kwa Bwana na jinsi nilivyokuwa nikiipata kiuhalisia katika mwili wangu na roho iliyokuwa imeteswa. Kwa kweli ilikuwa ni hali njema! Nilikuwa sijawahi kuipata hali kama hiyo kamwe.

Kwa kiwango fulani, Bwana alinipatia nguvu ya kuendelea kusonga mbele katika kipindi cha changamoto zote za kumtunza Ray wakati alipozidi kuwa dhaifu. Nilikuwa nikifanya kazi, nilikuwa nikiwatunza watoto, na

kusimamia mambo ya kifamilia. Ninaamini kwamba Mungu anatupatia nguvu tunazozihitaji wakati tunapokuwa tumepungukiwa na nguvu hizo. Ilipofikia mwezi Agosti mwaka 1989 Ray alifariki dunia kutokana na ugonjwa wake. Ninatumaini kwamba alienda kuungana na Bwana.

Ingawa hii ilikuwa ni miaka migumu sana, katika kipindi ambacho maisha yangu yalikuwa pia ni changamoto, ukweli ni kuwa Mungu aliendelea kuwa mwema kwangu na akaniwezesha kuipita miaka hiyo na katika miaka hiyo Bwana amenifundisha masomo yenye thamani sana. Masomo ambayo Bwana alinifundisha yapo katika kitabu hiki katika sura zinazofuata, ambapo nimeandika ili kuwashirikisha wengine tumaini nililo nalo. Kuna mambo mengi sana katika sura hizo ikiwemo kumpata mume bora kabisa, na muujiza mkubwa kabisa wa Bwana wa kuyalinda maisha yangu wakati ambapo nilikuwa karibu kufariki kutokana na UKIMWI na magonjwa mengine nyemelezi. Bwana amekuwa mwema sana kwangu. Amekuwa ni Mwanga Uongozao ambaye hajaniacha wala kuniangusha. Kwa kadri ninavyoendelea kuishi basi kauli mbiu yangu imekuwa ni, “Sintakufa bali nitaishi, Nami nitayasimulia matendo ya Bwana” (Zaburi 118:17).

1

WIMBI KUBWA

Katika majira ya joto ya mwaka 1989, maisha yangu na ya familia yangu yalionekana kuwa yenye huzuni na kusikitisha. Maisha yetu yalikuwa yakikumbwa na kimbunga cha baharini, kilichokuwa kikitupiga, kikitunyanyasa, na kutuzamisha katika kilindi cha bahari. Ray alikuwa amefikia hatua ya kuwa na UKIMWI huku akiwa na matatizo ya uvimbe sehemu mbalimbali ujulikanao kwa lugha ya kitaalamu kama *Kaposi's sarcoma*; pia alikuwa na tatizo la mfumo wa kupumua na kupoteza kumbukumbu, pia akawa na matatizo kwenye mapafu yake, na hatimaye akawa na aina mbalimbali za maambukizi. Alihitaji kupata huduma ya uuguzi wakati wa mchana nilipokuwa kazini. Watoto wangu walikuwa wakitunzwa na bibi yao wakati nilipokuwa kazini. Jioni nilirudi toka kazini, nikapika chakula, nikawahudumia watoto, na nikamhudumia Ray, nikasimamia mambo ya nyumbani, nikajitahidi sana kuhakikisha hatumezwi na majanga yaliyokuwa yanatusibu katika maisha yetu.

Miezi michache kabla ya kifo cha Ray mwezi Agosti 1989, hali kwa ujumla wake ilizidi kuwa ngumu sana kwangu. Mimi na Ray tulikuwa tumetengana sana kihisia kutokana tatizo lake la kupoteza kumbukumbu kiasi kwamba mawasiliano yakawa dhaifu sana. Hakukuwa na namna nyingine yoyote ya sisi kutiana moyo. Nilikuwa nikifanya kazi yenye kunipa msongo wa mawazo, maana ilikuwa ni kazi ya kutoa ushauri kwa watu wazima na watoto. Kazi hii peke yake ilikuwa ni kazi yenye mahitaji makubwa ya kihisia, kwa hiyo shida za nyumbani kwangu ziliongezea uzito katika kazi yangu, kwa kweli wakati huo nilijiona kama ninayetunza watoto watatu badala ya wawili hii ni kwa kuwa Ray alikuwa dhaifu sana. Nilikuwa nikimpeleka mara kwa mara kuonana na daktari hasa kipindi alipokuwa hawezi kuendesha gari.

Nyakati za usiku zilizidi kuwa ngumu sana. Lakini kwa namna ya kushangaza, kuna nyakati za usiku Ray alikuwa anapata nafuu. Kuna wakati alikuwa akiamka na kuanza kutembeatembea ndani ya nyumba. Nilipomuuliza kuwa alikuwa anataka nini alikuwa akijibu kama mtu aliyechanganyikiwa. Wakati fulani niliamshwa na kelele na nilipoangalia nilimwona akiwa amedondoka kwenye ngazi. Kwa bahati nzuri hakuwa amejeruhiwa. Hivyo ikanibidi nyakati za usiku niwe ninaamka mara kwa mara ili kumwangalia na kwa sababu hiyo sikuwa nalala vizuri. Kwa kweli nilichoka sana.

Wakati wa usiku hatukuwa na msaada na badala yake tulikuwa tunawapata wauguzi kwa masaa machache wakati wa mchana. Wakati fulani katika siku za mwisho wa wiki dada yake na Ray alikuwa akimtunza ili kunisaidia, lakini mbali na hapo ni watu wachache tu waliopenda kufika kwetu kwa kuwa wengi wao walikuwa na maumivu sana mioyoni mwao.

Kadri Ray alivyozidi kuwa mgonjwa na kujikatia tamaa, basi nilizidi kuwa na mashaka, nikawa na msongo mzito wa mawazo, na nikawa mwenye hofu sana. Hali ya kukosa usingizi mzuri kwa kipindi kirefu ilianza kuniletea matatizo. Katika kipindi chenye changamoto kali za kihisia ambazo ni pamoja na kuamka usiku, kufanya kazi, kutunza watoto, kumpeleka Ray kwa madaktari, na kuisimamia nyumba yetu ili iweze kwenda, basi hapo nilianza kuona kama ninapigwa na wimbi kubwa, na hatimaye hilo wimbi lilizidi kupata nguvu, na lilionekana kuzidi kuwa na nguvu kila siku na kunielemea. Na ilionekana kana kwamba hilo wimbi hatimaye litanimaliza kabisa na kuniua au kunifanya nipate tatizo la mishipa ya fahamu. Hilo wimbi kubwa lilikuwa ni msongo wa mawazo na kuchoka kulikoandamana na upungufu wa rasilimali fedha. Pia kilikuwa ni kipindi cha kutisha kwa sababu VVU vilivyokuwa vikimmaliza Ray pia vilikuwa ndani yangu vikienea taratibu. Sikuwa nafahamu kama na mimi nitaanza kuugua magonjwa yanayoambatana na UKIMWI, na pia nilikuwa sijui hasa ni wakati gani nitaanza kuugua

kwa kuwa nilikuwa nimegundulika kuwa na VVU mwezi wa Oktoba mwaka 1988. Nilikuwa nikiwahofia sana watoto wangu, wana wangu walio wema ambao hawakuwa na hatia, nikawa ninajiuliza ni nani atakuwa mlezi wao kama nitakabiliana na kifo. Wakati huo huo nilikuwa nikitamani sana kuwaona watoto wangu wakikua na kufikia utu uzima.

Mtunga zaburi analia kwa kutamka maneno yanayofanana na hali niliyokuwa nikiipitia wakati huo. Zaburi ya 69 inasema,

Ee Mungu, uniokoe,
Maana maji yamefika mpaka nafsini. Ninazama katika matope mengi,
Pasipowezekana kusimama.
Nimefika penye maji ya vilindi,
Mkondo wa maji unanigharikisha.
Nimechoka kwa kulia kwangu,
Koo yangu imekauka (aya ya 1-3).

Katika maombi yangu nilimlilia sana Mungu nikiwa katika hali ya hofu na kuogopa. Nilimwomba Mungu anilinde ili nisipigwe na wimbi kubwa na nikamwomba anisaidie ili niweze kuitunza afya yangu hata kipindi ambacho afya ya Ray ilipozidi kuwa mbaya. Pamoja na kuwa Ray alikuwa amenisaliti mimi na familia yetu, kwa kweli tulikuwa na historia yenye mafungamano kati yetu. Niliendelea kupambana na dhamiri mbaya huku nikitamani kuishi na kutomfuata Ray kifoni kama ilivyokuwa kwa wajane wa zamani wa kihindi mashariki mwa India ambao waliwekwa kando ya waume zao waliofariki na kuzikwa pamoja nao. Hata hivyo, kulikuwa na nyakati ambapo niliona ni kana kwamba atatangulia kufa kisha na mimi nitafuata haraka au nitabakia nikiwa na afya kadri itakavyowezekana. Ilipofikia hapo kwa kweli nilitamani sana kuishi—na pia nilitamani apate pumziko la milele kutokana ugonjwa wake, maana niliona kwamba nikiwa peke yangu ni rahisi kujisimamia.

Mtunga zaburi anaandika hivi,

Uniponye na kunitoa matopeni,
Wala usiniache nikazama.
Na niponywe nao wanaonichukia,
Na katika vilindi vya maji,
Mkondo usinigharikishe,
Wala vilindi visinimeze
Wala shimo lisifumbe kinywa chake juu yangu (Zaburi 69:14-15).

Ninaamini kwamba kwa neema yake Bwana aliingilia kati na kuzuia anguko kutokana na wimbi kubwa la wakati huo.

Nimejifunza kwamba ninapopitia matatizo na majanga makubwa katika maisha yangu, yaani wakati ambapo ninaona kama ndio nipo mwishoni hali nikiwa katika maombi mazito, basi mara nyingi Mungu ameingilia kati na kunisaidia. Inawezekana Mungu asiingilie kati muda uleule niwapo katika maombi lakini amekuwa akinisaidia muda mfupi tu baada ya maombi yangu. Wakati nilipokuwa nikiendelea kuomba ili wimbi kubwa lisiniangushe, Ray alilazwa hospitalini na hivyo tuliweza kuonana na wahudumu wa afya wa jamii na kupanga namna ya kumwandaa kukabiliana na kifo chake. Akiwa chini ya huduma hiyo niliweza kumtembelea lakini huduma nzima ya kumtunza ilisimamiwa na wahudumu wa afya. Kwa kiwango fulani ni kama nilipata pumziko la kusaidiwa kumtunza Ray na wahudumu wa afya pale hospitalini. Nilitambua kwamba Bwana alikuwa ametenda mambo yote kwa mujibu wa wakati wake na kwamba aliniokoa kwa namna ya kipekee toka katika anguko la kupigwa na wimbi. Baada ya kuwa amelazwa pale hospitalini Ray alifariki baada ya wiki moja. Nilimshukuru Mungu kwa yote pamoja na kuwa nilikuwa nikipitia kipindi chenye msongo wa mawazo ambacho kingeliweza kunimaliza. Niliendelea kuwatunza watoto wangu, nikaitunza na afya yangu, na nikaanza kuijenga upya familia yetu ili iwe katika mkao unaostahili.

2

ZABURI YA 91

Katika mkutano wetu wa kikundi kilicho chini ya huduma ya “Mungu Amedhamiria Ushindi” tunapokea huduma ya kiroho na usaidizi kutokana changamoto za kihisia, pia tunakuwa na nafasi ya kuomba; kwa mujibu wa muktadha wa kibiblia huduma ya Mungu Amedhamiria Ushindi ilikuwa ndio huduma ya kwanza ya kiinjili na ya Kikristo inayohudumia waishio na VVU/UKIMWI nchini Marekani. Huduma hii ilianzishwa mwaka 1990 katika kipindi ambacho kulikuwa na hofu na utisho mkubwa kuhusiana na virusi vya UKIMWI na madhara yake. Huduma ya Mungu Amedhamiria Ushindi inatoa elimu ya VVU/UKIMWI, inasaidia waishio na walio athirika na ugonjwa huu wa kutisha, pia inatoa huduma mbalimbali katika ngazi ya kimataifa kuhusiana na elimu, shughuli ndogo ndogo za kiuchumi, huduma za kitabibu kwa watu waishio na VVU/UKIMWI, uanzishaji wa makanisa ambayo yanawajali na kuwakaribisha watu waishio na VVU/UKIMWI, pia huduma hii inatoa huduma nyingine mbalimbali. Mungu Amedhamiria Ushindi ni huduma inayozingatia amri za kibiblia za kuwatunza wajane na yatima ambao wameathirika na kudhuriwa na VVU/UKIMWI.

Wakati fulani tukiwa katika mikutano ya vikundi saidizi vya Mungu Amedhamiria Ushindi tulikuwa tukizijadili aya fulani za Biblia ambazo zina maana maalum kwetu sisi tunaoishi na VVU, na tuliona kwamba kwa wengi wetu Zaburi ya 91 ni zaburi nzuri ya ulinzi hasa tuwapo katika hofu na mashaka kutokana na hali ya kuishi ya VVU/UKIMWI. Zaburi hii inatoa faraja maalum na ya kipekee kwa watu wanaoishi na VVU au walio na UKIMWI. Tulipoanza kujadiliana juu ya baadhi ya aya za Biblia ambazo ni nzuri, basi wengi wetu tulikubaliana kuwa

aya nzuri ni zile zinazotutia moyo hasa tunapokuwa tukiugua.

Ufuatao ni uchambuzi wa kina wa Zaburi ya 91 na inatoa maelezo mazuri na maalum kwa mtu aliyegundulika kuwa na VVU.

Zaburi inaanza kwa kusema: Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi" (Nukuu za Maandiko ya Biblia zinatoka katika Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa – Kenya [Nairobi] na Tanzania [Dodoma]). Inaanza na ujumbe wa usalama na matunzo. Zaburi hii inaelezea juu ya ulinzi maalum wa Mungu kwa wale wanaomtafuta. Mtu aliyegundulika kuwa na VVU anajiona kuwa yupo katika hali mbaya ya kuweza kuugua, kufa, na kukataliwa na jamii. Kwa jinsi hiyo tunahitaji kupata mahali pa kimbilio hali tukiwa na hofu na changamoto nyingi. Tunapofahamu kwamba tunaweza kusema pamoja na mtunga zaburi kuwa "Nitasema, Bwana ndiye kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu nitakayemtumaini" (aya ya 2), basi hapo tunakuwa tumefika nyumbani mahali penye uhakika na utulivu wakati kukiwa na dhoruba. Ni rahisi kuona watu waishio na VVU/UKIMWI na ambao hawana imani kwa Mungu wanakuwa ni watu wenye hofu sana kila wanapokabiliana na vitisho vya kiafya kutokana na kuishi na VVU. Watu wengi wanaendelea kutafuta faraja ya kiroho toka katika vyanzo mbalimbali. Wale wanaoweza kumpata Yesu Kristo wana bahati sana maana wataipata faraja maalum toka kwake. Kuna fursa ya huduma kwa wale wanaowatafuta watu ambao bado hawajapata faraja wanayoitafuta.

Kadri tunavyozidi kusoma zaidi katika Zaburi ya 91, mwandishi anaandika hivi, "Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji, Na katika tauni iharibuyo" (aya ya 3). Yeyote anayeishi na VVU au UKIMWI anafahamu kikamilifu juu ya hiyo tauni iharibuyo jinsi ilivyo. Mara ya kwanza nilipoisoma Zaburi ya 91 baada ya kuwa nimegundulika kuwa na VVU mwaka 1988, nilifikiri kwamba Mungu alikuwa akitambua jinsi ugonjwa huu mbaya ulivyo. Niliona dhahiri kuwa Mungu *alifahamu* juu ya ugonjwa huu karne

nyingi sana zilizopita hata kabla haujatokea. Kuna usalama mkubwa sana ndani ya Mungu kiasi kuwa hakuna kitu kinachomshangaza.

Kwa kweli, hapa ndipo tunapofikia hatua ya kujiuliza namna ya kuitafsiri aya inayosema atakuokoa, na swali linakuwa je, (ataniokoa mimi?) kutokana na tauni iharibuyo. Mwanzo kabisa wa historia yangu ya kuishi na VVU kuna wakati nilitamani pasipo kuzingatia uhalisia kwamba nipate uponyaji—kwa muujiza—wa kuweza kuponywa VVU. Lakini kadri muda ulivyozidi kwenda na uponyaji ukiwa haujapatikana, basi nilitambua kwamba hali si rahisi kama nilivyokuwa nimefikiria hapo awali. Pia nilitambua kwamba kuna mambo mengi sana ambayo pia niliitaji kupata uponyaji ikiwamo tabia ya kutokuwa na upendo na ubinafsi, ambapo kwa mazingira mengine tabia hizo ni mbaya kuliko VVU na zina madhara sana. Ninaamini kwamba Mungu yupo katika mchakato wa kuwaponya watoto wake wote. Hata hivyo, mwanzoni sikuweza kuzitambua hoja muhimu za kiimani kama hizi. Kwa wakati huo nilichokuwa nakitarajia ni kupata uponyaji na kwa kweli bado nina tumaini hilo. Siwezi kukata tamaa. Bado kuna uwezekano wa kupatikana matibabu hapo baadaye ambayo ninaweza kuyatumia.

Pamoja na kuwa bado sijaponywa, ukweli ni kuwa Mungu amenifanyia miujiza mingi katika maisha yangu. Pamoja na kuwa bado sijapata tiba, nimeuona muujiza wa kuishi maisha marefu. Hii inanionyesha kuwa Mungu anatuokoa kutokana na tauni iharibuyo kwa namna zake za kipekee.

Tunapoendelea kuiangalia Zaburi hii, aya ya 4 inatupatia picha nzuri ya ulinzi na matunzo. “Kwa manyoya yake atakufunika, Chini ya mbawa zake utapata kimbilio…” Kuku mwenye vifaranga huwakumbatia watoto wake chini ya mbawa zake zenye joto, mahali ambapo watoto huwa salama mbali na hatari na mashambulio yote. Ni mahali gani sasa ambapo ni pazuri zaidi ya kuwa chini ya umilele wa muumbaji anayejua yote mwenye kutushikilia ili tuwe karibu naye! “Hofu ya

usiku” inayotajwa katika aya ya 5 inaonyesha ni hofu ya kutomjua Mungu, ni hofu ya kutokuwa na Mlinzi, na ni hofu ya kushughulikia changamoto za VVU ukiwa peke yako. Mara nyingi hofu na kitisho huonekana kujidhihirisha zaidi nyakati za usiku. Ninakumbuka kwamba mara ya kwanza nilipogundulika kuwa na VVU nilikabiliana na hofu kubwa sana nyakati za usiku. VVU inaufanya uso wa mtu uwe ni uso wa mauti na hilo linaifanya safari ya kimaisha kuwa ya kutisha sana.

Kwetu sisi tunaoishi na VVU au UKIMWI, aya ya 7 ni neno kubwa sana linaloweza kuhusianishwa na idadi ya virusi katika miili yetu—“Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe.” VVU inaweza kuua, lakini tukiwa na Mungu VVU haiwezi kutuangamiza. Tunao uzima wa milele ambao hauwezi kuporwa na kitu chochote kile! Hivyo tunaweza kusema kwa ujasiri kwamba, “kama ukimfanya Aliye Juu kuwa makao yako, —yaani Bwana aliye kimbilio langu—basi hakuna madhara yatakayokupata wewe...” (aya ya 9).

Tukiendelea kuiangalia sura hiyo, tunafikia hatua ya kusema kiroho kwamba, “Kwa kuwa atakuagizia malaika zake Wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua, Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe” (aya ya 11-12). Maelezo haya yana nguvu sana inayoonyesha juu ya huduma ya Mungu kwa watu wake kiasi kuwa Shetani alizitumia aya hizohizo wakati alipokuwa akimjaribu Yesu, yaani wakati Yesu alipokuwa amekwenda jangwani ili kufunga na kuomba. Shetani alitambua nguvu iliyomo katika maneno haya yanayoonyesha nafasi yetu katika moyo wa Mungu. Ni maneno makuu sana yanayofariji watu wanaoteseka, yanaonyesha kuwa Mungu atawatuma viumbe wake wa kiroho kuja kwetu ili kutulinda dhidi ya uharibifu.

“Utawakanyaga simba na nyoka, Mwana-simba na joka utawaseta kwa miguu." Aya ya 12 na ile ya 13 zinatuonyesha kwamba sisi ni washindi halisi, na

kwamba nguvu za Mungu ndizo zilizo kuu kushinda yote. Kifo hakitaweza kamwe kutushinda.

Aya mbalimbali zinazofuata zinaelezea juu ya ukuu wa Mungu, uaminifu wake, na uwepo wake katika maisha yetu. Zinaonyesha juu ya ukuu na heshima tuliyo nayo. Kisha aya ya mwisho inatupatia tumaini jingine. “Kwa siku nyingi nitamshibisha, Nami nitamwonyesha wokovu wangu.” Je, hii ina maanisha kwamba tutaishi kwa muda mrefu, kama nilivyoishi miaka 22 tangu nilipogundulika kuwa VVU, miaka ambayo Mungu amenipatia, au je, hii ina maanisha kwamba tutaupata uzima wa milele? Je, hii inajalisha? Kwa kweli kama ambavyo nimekuwa nikiwaza, katika Kristo, mabaya katika maisha yangu yamefanywa ili kunipatia mema zaidi.

KUMKASIRIKIA MUNGU

Halikuwa kosa la Mungu lililofanya Ray aniambukize virusi vya upungufu wa kinga mwilini. Mungu hakuwa amesababisha dhambi iliyosababisha matokeo mabaya kama haya. Hata hivyo, kama Mkristo niliomba tena na tena ili Mungu aliondoe hili pigo la kutisha katika maisha yangu na hakufanya hivyo. Nilikuwa na hasira sana kuona kwamba maisha yangu hayaendi kwa namna nilivyotarajia na ilionekana ni kana kwamba Mungu alikuwa hanisaidii sana.

Niliteseka kutokana na fikra ya muumini isiyo sahihi kuwa Mungu alikuwa anastahili kuniokoa kwa kuwa nilikuwa nimeyatoa maisha yangu kwake. Niliamini kwamba kulikuwa na kila sababu ya mimi kulipwa kutokana na wema wangu. Nilitaka Mungu ayatatue matatizo yangu na kuyaweka maisha yangu yawe bora kikamilifu. Ni wazi kuwa waamini wengi tangu hapo zamani walikutana na mateso makubwa ambayo Mungu kwa mafumbo yake alikuwa ameyaruhusu. Lakini kama mwamini ambaye nilikuwa bado sijakomaa kwa kweli nilitamani kuwe na muujiza ambao ungenifanya nisisikie maumivu. Katika fikra zangu nilikuwa wakati wote nikivifikiria vifungu vya maandiko ambavyo vingeliweza kunipatia suluhisho la haraka. “Nawe utajifurahisha kwa Bwana, Naye atakupa haja za moyo wako” (Zaburi 37:4). Kwa hakika nilitamani sana kuwa huru mbali na mateso. Pia nilisoma mstari unaosema hivi, “Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea” (Mathayo 21:22). Nilifahamu kuwa nilikuwa nikiamini na hivyo nilitaka kupokea kile nilichokua nikikiomba katika sala. Pia kulikuwa na kifungu kingine mashuhuri, “Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa;

tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa" (Luka 11:9). Kwa kweli mimi sikubisha mlango bali nilikuwa nikiubamiza mlango.

Kwa upande wangu vifungu hivi vya maandiko vilionekana kuwa ni kama ahadi ambazo ningeliweza kuzihesabu kwa urahisi tu, yaani kwa namna ya vipimo vya kawaida tu. Lakini nimefikia hatua ya kujifunza kwamba kuna vipimo vingi sana tunavyovipitia katika mapito yetu hapa duniani na kwamba maombi yetu yamekuwa yakijibiwa si kwa namna ambavyo tumekuwa tukitaka yajibiwe. Bwana anajibu maombi katika namna ambayo imenifanya niweze kukua na si katika namna ambayo ingenifanya niendelee kudumu katika hali ya kutokukua na kudumu katika ubinafsi. Kwa kweli tendo la kuomba ili uweze kukombolewa toka katika maumivu si tendo la kibinafsi, lakini Bwana anaweza kuruhusu mateso kwa sababu mbalimbali ambazo hatuzifahamu na hufanya hivyo kwa ajili ya kutuletea mema.

Hivyo, kwa baadhi ya nyakati, hali nikiwa ni mjane na mzazi niliye peke yangu huku nikikabiliana na afya iliyokuwa inazorota, kwa kweli nilikuwa nakasirika sana, tena sana. Niliona hali nzima kwa ujumla wake ikiwa hainitendei haki. Sehemu ya hasira ilikuwa kwa Ray aliyeniingiza katika hali mbaya niliyokuwa nayo wakati ule. Lakini pia nilikuwa namkasirikia Mungu. Nilikuwa namkasirikia Mungu kwa sababu yeye Mungu alikuwepo na Ray alikuwa ameshafariki, nilikuwa na hasira kwa Mungu kwa sababu hakuyafanya maisha yangu yawe mepesi. Kulikuwa na hasira nyingi sana ikimiminika toka kila pembe ya maisha yangu kiasi kwamba nilihitaji mahali pa kuweza kusema ili nipumue la sivyo ningelipasuka.

Mara ya kwanza nilikuwa ninaogopa kumkasirikia Mungu Muumbaji wa ulimwengu. Niliona ni kana kwamba ningelikuwa sifanyi vema. Nilikumbuka hadithi ya Ayubu katika Biblia na jinsi alivyomuuliza Mungu. Mwishoni mwa kitabu cha Ayubu Mungu alimrudishia Ayubu nafasi yake pasipo shaka yoyote na alimuuliza. "Ulikuwa wapi

nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema, kama ukiwa na ufahamu. Ni nani aliyeamrisha vipimo vyake, kama ukijua?" (Ayubu 38:4-5a). Kwa hakika Mungu ni mkuu kuliko sisi na kuna mambo mengi sana ambayo hatuyafahamu kuhusu mipango yake ya kimungu. Lakini mapito yote niliyopitia hayakunifanya niache kumwelezea Mungu ukweli wa moyo wangu kwa kuwa kuna namna nyingi ambazo Mungu anatumia kutualika ili tuwe naye pamoja katika faragha na ushirika kwa kweli.

Kadri nilivyokuwa nikiomba na kutafakari kuhusiana na hitaji langu na kuwa na ushirika na Mungu, basi mara nyingi nilifikiria juu ya uhusiano ambao Mungu Baba alikuwa ameuumba, ambao ni uhusiano wa ndoa. Katika ndoa mara nyingi tupo huru kuelezea hasira zetu ili wapendwa tunaoishi nao waweze kufahamu pale ambapo tumekwazika au pale ambapo tumeumizwa. Pia nilitambua kwamba Yesu Kristo alitumia mfano wa ndoa katika kuelezea uhusiano wake na Kanisa. Katika kitabu cha Waefeso, mwandishi analinganisha uhusiano wa Kanisa na Kristo na uhusiano katika ya wanandoa. "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno" (5:25-26). Nilifikiria kwamba ikiwa ndoa ndio mfano wa Kristo na Kanisa Lake, basi mimi kama mwanachama wa huo mwili ninaalikwa kuwa na ushirika na Bwana kwa kina. Pia Yohana Mbatizaji alitumia lugha ya picha ya Kristo na Kanisa Lake kumaanisha ndoa pale aliposema hivi kiunabii, "Aliye naye bibi arusi ndiye bwana arusi; lakini rafiki yake bwana arusi, yeye anayesimama na kumsikia, aifurahia sana sauti yake bwana arusi" (Yohana 3:29). Mume na mke wana mahusiano ya ndani sana ambayo Mungu alikuwa ameyapanga katika uumbaji wa kidunia.

Nilipokuwa nikitafakari vifungu hivi vya Maandiko, nilitambua kwamba Bwana anatualika tuweze kuwa karibu naye kihisia na kiroho. Kwa kweli mambo haya mawili hayawezi kamwe kutenganishwa. Hisia ni sehemu ya maisha yetu ya kiroho. Nilianza kutambua kwamba ninaweza kumshirikisha Yesu sawa na nilivyokuwa nikimshirikisha

mume wangu alipokuwa angali hai yaani katika nyakati nzuri na nyakati ngumu. Ka kweli kulikuwa na tofauti ya kuwa na Mwokozi mwenye upendo ambaye ningeliweza kumshirikisha mambo yangu badala ya kuwa na mwanadamu mwenye mapungufu. Lakini ule ukweli kwamba Biblia inayalinganisha mahusiano yetu na Bwana na mahusiano ya ndoa, basi ukweli huo ulinipatia ujasiri kwamba Bwana ataisikiliza hasira yangu, na atayafahamu maumivu yangu kwa kina.

Hatimaye nilihitimisha kwamba kuna nyakati katika ndoa yangu niliwahi kumshirikisha mume wangu hasira zangu, basi kwa namna ile ile nitamshirikisha Mungu hasira zangu. Ninakiri kwamba pamoja na kuwa nilimwelezea Mungu juu ya hasira zangu, kuchanganyikiwa, ghadhabu, na maumivu yangu ya kina, ukweli sikuwahi kumtuhumu wala kumlaani Mungu. Kulikuwa na haja ya kuelezea machungu yote kwa namna yenye heshima. Nililia, nilipiga yowe, niliomba, na niliomboleza hadi nilipoona kwamba walau kwa kiasi fulani kulikuwa na pumziko ndani yangu. Niliona kwamba Mungu alikuwa amenisikia, na kwamba alikuwepo wakati nikipitia hali ile, na kwamba alinipatia faraja ya kihisia na kiroho katika majeraha yangu. Ilionekana kwamba Bwana aliweza kuyapokea mengi niliyokuwa nikiyatoa mambo ambayo watu wengine walio karibu nami wasingeliweza.

Tangu wakati huo nimekuwa mtu wa shukrani sana kwa fursa niliyoipata ya kuwa karibu sana na Bwana. Hatuna siri za kumficha Mungu na kwa sababu hiyo tunaweza kuongea naye kuhusiana na udhaifu wetu kimaadili, tabia zetu za dhambi, na mambo yote yanayotukatisha tamaa. Mara nyingi nimekuwa nikisahihiswa na Mungu kwa namna ambayo si ya kudhalilisha wala ya kunifanya nishindwe. Njia ya Mungu imelenga katika kunifanya niwe mnyenyekevu na si kunidhalilisha. Hata pale nilipokuwa sifikirii kuwa Bwana yupo, ukweli nilitambua kuwa yupo na kwamba atanisaidia na kunitia moyo katika maisha yangu.

4
UGUMU WA KUSAMEHE

Februari mwaka 1988, wakati Ray alipogundulika kuwa na ugonjwa ujulikanao kama *pneumocystis carinii pneumonia*, ambao ni moja kati ya magonjwa nyemelezi ya UKIMWI, kwa kweli nilipatwa na pigo kubwa mara tatu. Kwanza nilitambua juu ya hali yake ya kuugua kwa muda mrefu. Pili, nilitambua kuwa alikuwa ametusaliti katika ndoa yetu. Tatu, nilikuwa na mashaka kwamba hata mimi nitakuwa nimeambukizwa na VVU kupitia kwake. Ninakumbuka wakati akiwa amelazwa hospitalini na mimi nikiwa nyumbani, kwa kweli mara nyingi nilikuwa nikiamka kwa hofu nyakati za usiku, huku nikihofia kile kilichokuwa ndani yake; na huku nikihofia maisha ya wanafamilia wetu na mimi mwenyewe. Tulikuwa na watoto wazuri sana wawili ambao wangeliteseka kwa sababu ya usaliti huu na ambao wangeliweza kuwa yatima muda si mrefu; hii ni kwa sababu wakati huo watu waliokuwa na UKIMWI katika hatua yake ya mwisho waliweza kuishi kwa mwaka mmoja au miaka miwili tu. Nilifikiria kwamba hata mimi nitafikia hatua hiyo muda si mrefu, na hivyo kuwaacha watoto wangu pasipo mzazi wakati wakiwa bado wadogo. Nilijiuliza kama nitakufa ni nani atakaye walea.

Miaka mitatu baadaye, yaani mwaka 1991, dada yangu aliolewa. Nilifurahi sana kuona akiingia katika hatua nyingine ya kimaisha. Wakati huo huo nilikuwa na huzuni sana kwa kuwa maisha yangu yalikuwa yamevurugika na kwamba sikuwa na tumaini la kuweza kufikia ndoa yenye upendo na nidhamu ambayo nilikuwa nimeitamani kwa muda mrefu.

Nilipoolewa kwa mara ya kwanza niliamini kwamba maisha yangu “yatakuwa ni furaha daima;” lakini nilishuhudia hiyo ndoto yangu ikivunjika katika hali ya kukatisha tamaa hali nikiwa mjane ninayeishi na VVU huku nikiwa na wajibu wa kuwatunza watoto wangu wawili wadogo. Maisha yangu yalionekana kuwa na majeraha sana kiasi kwamba wakati mwingine nilifikiria kuwa yatosha kuishi.

Pia nilikuwa na mzigo mkubwa wa hasira na uchungu ambao ulikaribia kunivunja, maana vitu hivyo vilikuwa vimerundikana sana kama vile theluji inavyolundikana barabarani wakati wa kipindi cha baridi kali. Nilitambua kwamba nilikuwa na jukumu la kuishinda hasira hiyo ingawa mara nyingi ilionekana kana kwamba haiwezekani.

Nilipokuwa nikiyasoma Maandiko, nilikutana na mfano wa Yesu ambao unaelezea juu ya mtu aliyeshindwa kusamehe katika Mathayo 18:21-34. Kulikuwa na tajiri aliyekuwa akidaiwa deni kubwa ambalo hakuweza kulilipa hivyo akasamehewa deni lile na bwana wake. Kisha huyo tajiri aligeuka na akakataa kusemehe deni dogo ambalo alikuwa akimdai mtumishi wake. Katika mfano huu, Yesu anatueleza kwamba yule tajiri alipelekwa kwa msimamizi wa gereza ili ateswe kutokana na namna alivyomtendea mtumishi wake. Yesu aliwaeleza wasikilizaji wake kwamba, “Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake” (Mathayo 18:35). Pamoja na hayo kwa kweli sikupenda kabisa kusamehe. Nilikuwa nimepewa mlima wa kuuchimba na kwa kweli haikuwa haki kwangu mimi na kwa watoto wangu. Sikupenda kushughulikia matatizo ambayo nilikuwa nimeletewa. Kwa upande wangu, msamaha ungelimaanisha kuwa Ray “ameondoka katika ndoana.”

Nilipokuwa nikisoma zaidi Maandiko yalinionyesha amri makini kabisa. Mathayo 6:14-15 inasema, “Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali

msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." Ilipofikia hapo ilionekana dhahiri kwamba kama nilitaka kuendelea kuishi kwa neema ya Mungu basi kulikuwa hakuna namna ya kukwepa jukumu hili la msamaha.

Basi hapo nilianza safari kuelekea msamaha ambayo ilikuwa ni safari ya miaka mingi. Kwanza kabisa ilinibidi niombe kupata nia thabiti ya kuweza kusamehe kwa kuwa sikuwa na nia hiyo. Kulikuwa na semina ambayo iliendeshwa na wanasaikolojia wawili wa Kikristo ambao Dkt Henry Cloud na Dkt John Townsend ilinipatia mwanga mzuri sana na hivyo kuweza kufungua milango ya moyo wangu usiosamehe. Katika semina ile walifundisha kwamba tunapokuwa hatujawasamehe wengine, basi huwa bado tumefungwa na watu hao kama vile mpira na mnyororo. Bila msamaha tunaendelea kuhusianishwa nao kifikra kwamba wanadaiwa na sisi na kwamba hatutaki kuwaweka huru. Mtazamo huu unatufanya hata sisi tusiwe huru, na hivyo kufungwa na watu wengine na hivyo kuburuzwa katika njia yenye chuki. Matarajio yetu huwa ni kwamba mtu mwingine naye ajitahidi kufanya vizuri kwa usahihi. Ni vigumu kutegemea watu wafanye hivi wanapokuwa wangali hai, na ni jambo lisilowezekana kabisa kwa watu kufanya hivyo wanapokuwa wameshatoweka duniani. Kwa maelezo hayo ilikuwa ni dhahiri kuwa hasira na majuto yangu vilikuwa havina faida zaidi ya kuendelea kuniumiza tu.

Hali yetu ya kutokusamehe inatufanya tuwe na muungano kihisia na mtu mwingine, na kwa upande wangu kulikuwa hakuna sababu ya kuendelea kuwa na muungano wa kihisia na mtu ambaye alikwishaondoka katika maisha yangu. Kuna watu ambao kwa kupitia hisia zao wanaungana na roho na mizimu ya kila namna, kama vile mume mtarajiwa, mume wa kufikirika tu, na tabia ya "ikiwa tu," n.k. Hivyo nilipaswa kuachana na fikra hizo hasi. Matunda yatokanayo na tabia hiyo ni mateso na uchungu na hivyo kupata maumivu zaidi. Kwa kweli haikuwa rahisi lakini hatimaye niliona kwamba Mungu angeliweza kushughulika na Ray milele na

kwamba jukumu langu ilikuwa ni kumwachilia. Nilizidi kuomba tena na tena ili niweze kusamehe na hatimaye niliweza kusamehe na vifungo vya kihisia viliniondokea.

Jambo la muhimu ambalo nililitambua ni kwamba hata mimi sikuwa ninastahili kupata msamaha wa Mungu, lakini Mungu alinipatia msamaha bure. Sasa ninawezaje basi kuuonea gere msamaha wa Mungu kwa mtu mwingine? Mungu anafahamu yote ni Muumbaji na ana uwezo mkubwa kuitambua mioyo ya watu kuliko mimi, lakini Mungu anawasamehe wauaji, wezi, na watenda maovu. Kwa kweli ninamshukuru Mungu kwa zawadi ya msamaha wenye neema!

Mbali na ule uhuru wa kufunguliwa minyororo ya kihisia, baada ya miaka kadhaa Mungu alinibariki kumpata mume mcha Mungu anayetambua kwamba ninaishi na VVU lakini ananipenda sana hali nikiwa na hali hiyo. Mungu aliuangalia moyo wangu na nafsi yangu kupitia VVU. Mungu aliyajibu maombi yangu yaliyokuwa kana kwamba hayawezekani, yaani maombi ya kuolewa na mtu mwenye upendo na mwenye nia ya dhati. Ninapofikiria miaka ile ya 1991 na jinsi nilivyokuwa katika maumivu, kwa kweli ninachoweza kufanya ni kumshukuru Mungu tu ambaye alinivusha katika safari iliyokuwa na changamoto nyingi ikiwemo kusamehe.

5
KWA NINI IWE MIMI?

Swali linalojirudia rudia kwa wengi wetu tunaosumbuliwa na maambukizi haya ni, “Kwa nini iwe mimi?” Nilikuwa nikimuuliza Mungu swali hilo mara kwa mara. Kwa nini nilipata UKIMWI wakati nilikuwa sijafanya mambo mabaya kama vile kujidunga madawa ya kulevya au kufanya mapenzi nje ya ndoa? Niligundulika kuwa na maambukizi ya VVU wakati nikiwa Mkristo. Ni kwa nini Mungu aliruhusu mwana wake kupata ugonjwa wa kutisha kama huo? Nilikuwa nikijiuliza maswali kama haya pamoja na wenzangu kwa miongo mingi.

Maswali kama haya yamekuwa yakiulizwa na watu wengi tangu mwanzo wa mwanadamu. Ninapomtakafari Adamu ninaona akisema, “Bwana, kwa nini iwe mimi? Huyu mwanamke uliyenipa ndiye aliyenipa tunda nikala.” Na bila shaka Hawa naye atakuwa alisema, “Bwana, kwa nini iwe mimi? Ni shetani ndiye aliyenidanganya.” Asili yetu ya kibinadamu inataka iwe huru mbali na matokeo yasiyofurahisha kwa kuwa tunapenda maisha yetu yawe rahisi na yenye furaha, yaani maisha yasiyo na maumivu. Lakini mara nyingi uhalisia wa maisha hauko hivyo.

Filamu moja iliyokuwa na maudhui matamu na machungu iliyoitwa *Ndugu Holland Opus* inaelezea juu ya hadithi ya kweli ya maisha ya mwanamuziki aliyekuwa na ndoto za kutengeneza muziki wa aina ya simfoni utumiao ala nyingi za muziki, lakini hakuweza kufikia malengo yake kwa kuwa kuna shida nyingi za kimaisha zilizochangia kuvuruga ndoto zake. Jambo la kushangaza, huyu mtu aliyekuwa anapenda sana muziki alikuwa na mtoto mwenye ulemavu wa kusikia, yaani kiziwi. Kadri ndugu Holland alivyokuwa akiendelea kupiginia ushindi wa ndoto zake na

kunung'unikia mambo aliyopoteza, alifikia mahali ambapo maisha kwa ujumla yake yalimtupa mkono. Katika tukio moja linalovutia, huyu ndugu aliimba wimbo kwa heshima ya mtoto wake. Ni wimbo ulioimbwa na John Lennon na unasema hivi, "Maisha ni kile kinachotokea wakati ukiendelea kufanya mipango mingine." Kwa kweli kuna ukweli wa kutosha kabisa katika ubeti huu wa muziki.

Sisi ambao tumetupwa na kutolewa nje ya barabara za kimaisha kwa kutotimiza ndoto zetu mara nyingi tunashindwa kuzizuia hisia za hasira, kuchanganyikiwa, na wakati mwingine hisia za uchungu. Mara nyingi huwa tunamlilia Mungu tukisema, "Kwa nini? Kwa nini itokee hivi wakati nikiwa Mkristo? Ni kwa nini iwe ni wakati ambapo nilikuwa nimeyaweka maisha yangu vizuri? Ni kwa nini itokee wakati nikiwa nimefunga ndoa? Ni kwa nini itokee wakati huu nikiwa na mtoto? Maswali ya namna hiyo huwa mengi sana.

Maandiko yanatusaidia kuyafahamu mafumbo ya uundaji wa Mungu na asili ya mwanadamu. Kwanza, tunafahamu kwamba tunaishi katika ulimwengu ulioanguka na usio mkamilifu. Biblia inasema, "maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki" (Mathayo 5:45b). Njia panda kuu katika maisha ni ule ukweli kwamba watu wema hawako mbali na bahati mbaya. Lakini ukweli mwingine ni kwamba hata hao watu wema wanatenda dhambi na wanapungukiwa na mapenzi ya Mungu.

Hata hivyo, bado hatujaweza kulijibu swali la "Ni kwa nini?" Kwa kweli Ayubu alimuuliza Mungu swali hilo hilo na akapokea majibu yafuatayo. "Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema, kama ukiwa na ufahamu" (Ayubu 38:4). Kwa maneno mengine, hatuna uwezo ya kuyatambua mafumbo yote ya Mungu katika maisha yetu. Kwa kweli hatuwezi kumfahamu Mungu kikamilifu kwa kuwa Mungu ni mkamilifu na mwenye uwezo usio na mipaka. Yeye ndiye aliyeumba ulimwengu, na kwa kweli njia zake si njia zetu sisi. Kwa kweli ninajifunza kuridhika na kuifurahia hali ya kutoridhika na mafumbo ya Mungu.

Pamoja na yote, ninamtumaini Mungu na ninafahamu kuwa ananipenda; na kwa sababu hiyo ninaweza kupumzika kutokana na ukweli huo hata kama ninapitia mateso.

Pili, Yesu anatupatia uelewa kuhusiana na swali la “Kwa nini?” hasa katika ile hadithi ya mtu aliyekuwa amezaliwa kipofu. Biblia inasema, “Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?” (Yohana 9:1-2). Hili lilikuwa ni aina ya swali la “kwa nini”. Kwa maneno mengine, kwa nini mtu huyu alikuwa akiteseka na upofu? Kwa nini alitenda makosa au kwa nini wazazi wake walitenda makosa kiasi cha kumfanya azaliwe kipofu? Yesu alijibu, “Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake” (aya ya 3a).

Huyo kipofu alikuwa ni mtu aliyekuwa akiteseka. Hakuwa amefanya jambo lolote lililomfanya astahili kupata shida hiyo. Hivyo, Mungu hamwadhibu Mkristo ambaye ameshayatubia makosa na dhambi zake za zamani wakati anapokuwa na VVU. Pamoja na kuwa VVU ni matokeo ya tabia ya dhambi, ukweli ni kuwa VVU si adhabu. VVU inaweza kuwaangukia na kuwapata wasio na hatia, waliosamehewa, na wenye dhambi pia. Na katika kipindi chetu cha kimaisha kama Wakristo mara nyingi huwa tunajikuta tukiwa katika moja kati ya makundi hayo matatu.

Mwishowe katika hadithi inayomhusu yule kipofu Yesu alitoa nuru inayolijibu swali la kwa nini kwa namna inayopendeza. Yesu akasema, haya yametokea ili “…kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake" (aya ya 3b). Yesu alimponya yule kipofu ili yeye pamoja na watu wengine waweze kuona zawadi nzuri ya Yesu Kristo—ambayo ni upendo wake, huruma zake, ukuu na nguvu zake.

Sasa, ninapotaka kuliuliza swali la kwanini, basi huwa ninafikiria sana juu ya **miujiza** mingi ambayo Mungu amenitendea katika maisha yangu. Huwa ninafikiria juu ya upendo wake wa ajabu. Mara nyingi huwa ninashangazwa na yale ambayo Mungu ameyafanya na anaendelea kuyafanya

kwangu. Ikiwa Mwana wake pekee hakuzuiliwa kwenda msalabani, basi ni kwa nini mimi nisiyakubali mateso ambayo Bwana ameyaruhusu katika maisha yangu? Hivyo, ninapofikiria kuwa “Ni kwa nini iwe mimi?” basi huwa ninanyenyekezwa na Mungu wangu na kisha kujiuliza “Kwa nini isiwe mimi?”

6
KUITUPA TABIA YA HOFU

Kulikuwa na mtu mmoja mashuhuri sana katika kitabu cha katuni za kuchekesha ambacho kauli mbiu yake ilikuwa ni “Nihofie kitu gani?” Kauli mbiu hii ina maanisha kuwa mtu huyo aliendelea na maisha yake pasipo hofu na bila kujali matukio yoyote yaliyojitokeza. Kwa bahati mbaya, kauli mbiu hii ilionekana kutofanya kazi kwa upande wangu. Hii ni kwa kuwa katika maisha yangu nimetawaliwa sana na tabia ya hofu. Baadhi ya watu hutafuna kucha, na wengine huvunja vifundo vya vidole vyao, na katika yote hayo mimi huwa nahofia.

Nilionekana kuwa na imani isiyo dhahiri kwamba kwa kuhofia pengine ninaweza kubadilisha matokeo ya hofu yaliyokuwa yakinijia kutokana na hali ya kimaisha niliyokuwa nayo. Kwa kweli kilichotokea ni kwamba nilizidisha hofu na mashaka yangu pasipo kutatua tatizo hata kwa yodi moja.

Nikiwa yatima niliyefiwa na mume katika mwaka 1989 nilikuwa nimejiundia tabia ya hofu katika kiwango cha juu. Ulipofika muda wa kukilaza kichwa changu katika mto wa kulalia, basi nilianza kupatwa na hali ya kuchanganyikiwa nikiwa na hofu mbalimbali kuhusiana na mambo kama; fedha, watoto, kazi yangu, afya yangu, na hofu nyingine nyingi zisizo na mwisho. Basi hatimaye nilijikuta nikilala usingizi wenye uchovu na kisha kurudia hofu zilezile wakati wa asubuhi. Nilijikuta ninazama kwa kina katika tabia hiyo ya hofu na nikajikuta nikizingirwa na hofu hasa akili zangu zilipokuwa mbali na shughuli za kikazi au shughuli za kifamilia. Hofu ikageuka kuwa mzigo wenye kutesa na hatimaye nilitambua kwamba sintaweza kuendelea na mzigo huo wa hofu zaidi, kwa sababu niliona tabia hiyo inaongeza mashaka zaidi pasipo kutoa suluhisho la tatizo. Ninafahamu kwamba Biblia inatuonya juu ya kuhofia na hivyo niliamua

kutafuta msaada toka katika Maandiko ili niweze kuiacha tabia hiyo ya kuhofia.

Nilipokuwa nikifanya utafiti ili kupata mwangaza, niliona kwamba Zaburi ya 127 inatuonyesha juu ya umuhimu wa kumwachia Mungu ili aweze kushughulikia mashaka na hofu zetu. Mtunga zaburi anaandika hivi, “Kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema, Na kukawia kwenda kulala, Na kula chakula cha taabu; Yeye humpa mpenzi wake usingizi” (aya ya 2). Kwa kweli haya ni maelezo muhimu sana ambayo yanaendana na nilichokuwa ninakifanya katika tabia yangu ya kuhofia: yaani kwa kupoteza muda mzuri na wa kutosha wa kupumzika usiku. Bwana wetu hapendi tuhofie na kuwa na mashaka kwa sababu hilo si jambo lenye afya, vilevile Bwana anataka kutusaidia mambo mengi katika maisha yetu. Tunapohofia mara nyingi tunakuwa hatutoi matunda yoyote yale, na tunakosa afya nzuri, na mbaya zaidi tunashindwa kuutumia usaidizi wa Bwana katika maisha yetu. Hii haimaanishi kwamba hatupaswi kuweka mipango na kutumia akili katika kutatua matatizo yanayotukabili, bali maelezo haya yanathibitisha kwamba hofu mara zote haina matokeo bora, inaharibu, na inavunja moyo na kuturudisha nyuma. Biblia inasema, “Moyo wa mtu huifikiri njia yake; Bali Bwana huziongoza hatua zake” (Mithali 16:9). Tunapaswa kuweka jitihada katika kuweka mipango na kisha kusonga mbele lakini ukweli ni kuwa hofu haituwezeshi kusonga mbele kabisa. Pia tunapaswa kuiweka mipango yetu mbele za Mungu ili tuweze kuyatambua mapenzi yake.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake juu ya kuhofia katika hotuba yake kuhusu ndege wa angani ambao wanalishwa na Baba yao wa Mbinguni na juu ya maua ya kondeni ambayo huvishwa na Mungu. Yesu aliongeza kwa kusema kwamba sisi ni wenye thamani sana kuliko hao na kwamba Baba Yetu anataka kuyashughulikia mahitaji yetu zaidi na zaidi. Kisha Yesu akasema, “Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?” (Mathayo 6:27). Na ushauri wake busara ni

kwamba utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake. Yesu aliyasisitiza mafundisho yake kwa kusema, “Basi msisumbukie ya kesho (Mstari uliopigwa ni wa nyongeza ya mwandishi); kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake” (Mathayo 6:34).

Nilipozisoma hizo aya nilitambua kwamba ninapaswa kubadilisha tabia zangu, shida ikawa ninawezaje kubadilika kwa kuwa nilikwishazoea tabia hiyo ya kuhofia kwa kina. Kwa kuwa aya ilinipatia dondoo za muhimu, “Usiihofie kesho,” basi niliamua kushughulikia yale yaliyokuwa yakitokea leo tu bila kujali yanayohusu mwezi mzima, mwaka mzima, au miaka kumi. Kama nilipaswa kufanya uamuzi muhimu, basi nilifikiria kile ambacho ninaweza kukifanya kwa siku hiyo tu. Kwa mfano, mara baada ya mume wangu kufariki dunia nilipaswa kujaza fomu nyingi sana, na kuweka kiapo cha urithi na kujaza fomu nyingi za kisheria. Nilijiwekea nia ya kushughulia fomu ninazoweza kuzijaza kwa siku moja na kuachana na kuyahofia mambo ambayo sikuwa nimeyafanya. Kuna nyakati nyingi ambapo nilirejea katika tabia ya kuhofia na hivyo ilinichukua miezi kadhaa hadi kuweza kuachana na tabia hiyo huku nikijikumbusha kupitia Maandiko juu ya nia yangu ya kubadilika. Kila nilipokabiliana na hali ya kuhofia niliyageuza mawazo yangu kufikiria jambo jingine. Baada ya kitambo fulani na baada ya kuwa nimefanya maombi mengi sana, tabia hii ya kuhofia ilianza kutoweka taratibu na hatimaye ikapotea kabisa.

Jambo la pili ambalo nilipaswa kujifunza lilitokana na ukweli kwamba ikiwa sikuwa na uwezo wa kuibadili hali fulani, kama vile kuwa na VVU, basi sikupoteza muda wangu kulihofia hilo. Hata nilipokabiliana na majanga ya kiafya, basi nilitumia wasaa huo kuomba kwa Mungu ili kupata unafuu wa kifikra na kiimani. Hivyo kauli mbiu yangu ni, “Kama nikiweza kutenda, basi nitachukua hatua zinazostahili, kama siwezi kutenda, nitaomba.”

Hofu ni kitu ambacho bado ninaendelea kupigana nacho hadi leo hii kwa kuwa hujirudia rudia. Wakati changamoto mpya inapojitokeza, mara nyingi tabia yangu ya hofu hutaka kujirudia na kunitawala. Kwa sasa ninachofanya ni kuweka mipango, na kisha kuombea mambo na maisha yangu ya baadaye huku nikiyatafuta mapenzi ya Mungu, lakini ninajizuia kabisa kuhofia. Kwa kweli maombi ni nguvu muhimu sana katika jitihada hizi. Mara nyingi ninaona kwamba ninapogeukia maombi, basi mara nyingi matokeo huwa mazuri katika kuishinda hofu. Kuna wakati huwa ninapata picha ya kifikra kana kwamba ninauweka mzigo wangu katika mapaja ya Bwana na kisha kuuacha mzigo huo ukae hapo na ubebwe na nguvu zake aliye mwenyezi. Kuwa na VVU kuna maanisha kwamba nina maisha ambayo hayana uhakika wa baadaye na mara nyingi hali hiyo hunifanya nihofie hasa pale ninapokuwa na matatizo ya kifya au pale majibu ya vipimo vyangu vya kifya yanapokuja kinyume na nilivyokuwa natarajia. Lakini katika hali kama hiyo huwa ninajitahidi kurejea katika hali ya kawaida kwa kuiweka mizigo yangu katika miguu ya Bwana.

7
AIBU

Kamusi ya Webster inalitafsiri neno aibu kuwa ni fikra sumbufu itokanayo na dhamiri mbaya, au itokanayo na tabia mbaya. Ni neno baya sana! Lakini katika Biblia kuna mtazamo tofauti wa wale wanaomtumaini Mungu. Mtunga zaburi anaandika hivi, "Wakamwelekea macho wakatiwa nuru, Wala nyuso zao hazitaona haya" (Zaburi 34:5). Pia Daudi alimshangilia Bwana kwa maneno haya, Nimekukimbilia Wewe, Bwana, Nisiaibike milele..." (Zaburi 31:1).

Kutokana na uzoefu wangu wa kusafiri sehemu mbalimbali ulimwenguni, nimeona kwamba mara nyingi VVU vinahusishwa na aibu. Ni ugonjwa ambao mara nyingi unaulizwa uliupataje ili waweze kukupanga katika makundi ya mashoga, watumiaji wa madawa ya kulevya, au mwanamke kahaba. Maswali haya hayatoki kwa magonjwa mengine kama vile ugonjwa wa kansa au shambulio la moyo.

Sisi tunaoishi na VVU tunaishi na aibu kila siku iitwayo leo. Lakini, dhambi zetu zina tofauti gani na wale wanaotuzunguka? Je, dhambi zangu ni kubwa kuliko mume wangu asiyeishi na VVU? Kizazi cha wanadamu kinaishi na aibu kwa sababu ya hali ya anguko la mwanadamu. Lakini mara nyingi aibu hiyo inaondolewa pale tunapomwomba azifunike dhambi zetu kwa haki yake.

Aibu iliingia katika kizazi cha mwanadamu kuanzia kwa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Kwa kuwa walikuwa wamezuiwa wasile tunda la ujuzi wa mema na mabaya, na wao wakakaidi ndio maana walijificha mbele za uso wa Mungu kwa sababu ya aibu. Sasa, ni kwa nini Daudi alisema kwamba wale

wamtazamao Mungu hutiwa nuru, na kwamba nyuso zao hazitaona haya?

Kuna mchakato imara sana ambao Bwana ametupatia. “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote” (1 Yohana 1:9). Mungu ameumba sakramenti ya msamaha ili kwamba aibu yetu kwa tendo lolote la zamani, tendo la sasa, na tendo la baadaye iweze kufutiliwa mbali hasa ikiwa tumeziungama dhambi zetu kwake.

Bila shaka Mfalme Daudi alifahamu hilo. Yeye alikuwa ni mzinifu aliyekuwa ameamuru kuuawa kwa mume wa mke aliyekuwa amemtwaa—kwa kifupi alikuwa ni muuaji. Pamoja na hayo Daudi alijifunza kujinyenyekeza mbele za Mungu na kuomba toba.

Wengi wetu tunazitubu dhambi zetu halafu baadaye tunaendelea kuona aibu pamoja na kutambua kuwa tumesamehewa. Wakati mwingine kuna hatua zaidi ambazo zinapaswa kuchukuliwa. Hatua moja ambayo ni muhimu sana ni kujisamehe sisi wenyewe. Hii haijalishi kwamba tumefanya “dhambi kubwa” au “dhambi ndogo” ukweli ni kuwa dhambi hizo zote zipo kinyume na utakatifu wa Mungu. Mungu hana orodha ya dhambi mbaya ambazo zinapokea msamaha kwa asilimia 90% na wala hana orodha ya dhambi mbaya ambazo zinapokea msamaha wa asilimia 10%. Mungu ameahidi kutusafisha dhambi zetu zote kikamilifu.

Kinachotokea mara nyingi huwa ni tendo la kuendelea kujiadhibu wenyewe wakati tumekwishatubu. Lakini kutokana na muundo mkuu wa Bwana, bado tunaweza kumtazama tukiwa na “nyuso zilizojawa na nuru” na zisizo na alama yoyote ile ya aibu. Yesu Kristo aliichukua aibu yote tunayostahili.

Kwa kweli Bwana ni mwenye rehema na neema nyingi. Kuna wakati tunaweza kuona ni kana kwamba hatustahili kupata msamaha wake. Kimsingi, hatustahili. Lakini kwa upendo kabisa Bwana anatoa msamaha huo pale tunapokiri na kuzitubia dhambi zetu. Kwa kweli hilo

ni tendo kuu sana la upendo! Ikiwa Mungu ambaye ni mtakatifu tena na tena anaweza kutusamehe, basi ninaamini kwamba sisi nasi tunapaswa kujisamehe wenyewe na kuwasamehe wengine. Wakati mwingine inakuwa vigumu sana kutenda hivyo.

Ulimwengu unaweza kututazama sisi tunaoishi na VVU kama wakoma wa kipindi cha sasa, lakini ni wazi kuwa sisi wenyewe tunapaswa kutazamana na kisha kumtazama Bwana kwa nyuso zenye nuru. Neno nuru linatafsiriwa kuwa ni “utoaji wa miale yenye mwanga; kung’aa sana; kuonyesha raha, hali ya kuwa na furaha, n.k”

Je, ni kipi nitachukua kati ya aibu au nuru? Mimi nitachukua nuru!

8
DHAMIRI MBAYA

Sisi tunaoishi na VVU/UKIMWI na sisi ambao ni wazazi tuna kila sababu ya kujiona wenye dhamiri mbaya. Baadhi yetu tuliambukizwa kutokana na uchaguzi mbaya wa kitabia, wengine waliambukizwa kutokana na kumwamini mtu asiye sahihi, lakini sisi sote ambao ni wazazi tumekuwa tukiishi na madhara mabaya ya VVU/UKIMWI kwa watoto wetu.

Kuna wakati nilikumbana na hiyo dhamiri mbaya katika macho yangu. Ni wakati ambapo nilikuwa ninajisikia kuchoka sana na kupumua kwa shida, pia nilikuwa najisikia uzito kichwani, pia nilikuwa ninajisikia dalili nyingine ambazo ziliifanya afya yangu "kuyeyuka." Nilipowaendea washirika wenzangu wa maombi katika maisha yangu, na nilipowaeleza kuwa ninajisikia uzito katika kifua changu, waliniambia nimuulize Mungu juu ya kitu kinachofanya uwepo huo uzito katika kifua changu. Mara nikatambua kwamba uzito katika kifua changu ulikuwa ukitokana na hofu ya watoto wangu. Baadhi ya hofu na mashaka yangu vilikuwa ni: Ni kitu gani kitawatokea watoto wangu baada ya kuwa nimefariki dunia? Je, watoto wangu watakuwa na mahusiano na Yesu katika maisha yao? Watawezaje kukabiliana na changamoto za kumpoteza baba yao kutokana na UKIMWI na kisha kumpoteza mama yao ambaye wameishi naye kwa takribani maisha yao yote? Je, mizigo hii imewaathiri vipi wanangu? Nakadhalika. Naomba mfahamu kuwa kwa sasa watoto wangu wote wamekua, na wanajitegemea, lakini kuna wakati hofu kama hizi zinajitokeza na zilikuwa hazikomi.

Tulipokuwa tukiomba, wapendwa wanamaombi na washauri walinikumbusha kwamba watoto ni mali ya Yesu, na kwamba Yesu atawatunza na kushughulika nao. Rafiki yangu aliniomba akitaka nimwombe Bwana kuwa mrithi wa watoto wangu mara nitakapoondoka duniani, bila kujalisha kama ni mwaka mmoja tangu wakati huo au ikiwa itakuwa ni miaka ishirini ijayo. Wakati huo watoto wangu wote walikuwa wamemkiri Yesu kuwa ni mwokozi wao; walikuwa wamebatizwa wote, ingawa wengine walikuwa hawahudhurii kanisani mara kwa mara, basi ndio maana nilikuwa na hofu ikiwa watoto hawa wana imani thabiti na tumaini katika Yesu. Lakini kama Biblia inavyosema: “Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua...” (Yohana 10:14). Kwa kweli wanangu ni mali ya Yesu, hivyo sina hofu ya kuhofia. Kwa kweli sijakata tamaa ya kuendelea kuwaweka mikononi mwa Bwana. Lakini kitendo cha kujaribu kubeba mizigo ya watoto wetu kuhusiana na maisha yao na Bwana ni jambo ambalo hatuwezi kulifanya; ni Yesu tu ndiye anayeweza. Yeye ndiye Mchungaji wao.

Niliomba na kuwaacha mikononi mwa Bwana na katika hali ya kushangaza, ule uzito uliokuwepo kifuani kwangu uliondoka. Nililia kwa furaha baada ya kutambua kwamba ninaweza kuiweka mizigo yangu niliyokuwa nikiibeba; mizigo ambayo nilikuwa nashindwa kuibeba, yaani mizigo ambayo sikupaswa kuibeba. Yesu alisema, “kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi” (Mathayo 11:30). Pamoja na hayo bado Bwana alikuwa hajaachana na mimi.

Wiki moja baadaye, niliweza kuomba pamoja na wanawake wawili ambao nilikuwa nimewaalika nyumbani kwangu ili waweze kuniombea katika maombi mazito, yaani sala nzito sana, kwa ajili ya uponyaji zaidi. Tulipokuwa tukiomba mwanamke mmoja alisema amepata ujumbe toka kwa Bwana kwamba nilikuwa nikiwafikiria sana watoto wangu. Na wakati huo nilikuwa sijamweleza chochote kile maana nilikuwa nimechoka sana, hivyo nilishangazwa sana nilipoona kwamba Roho

Mtakatifu amempatia ukweli huo. Hivyo nikaanza kulia na nikamweleza juu ya yaliyojiri nilipokuwa katika kipindi cha maombi wiki moja iliyopita. Nilifikiri kwamba mzigo umeondolewa, hivyo nikatambua kwamba maombi yalikuwa bado yanahitajika. Basi yule mama alipokuwa akiomba alimwomba Bwana aondoe fikra zozote za dhamiri mbaya katika moyo wangu. Hapo nilianza kulia kwa machozi mengi sana; maana ni wakati huo ndipo nilipotambua kwamba nilikuwa najisikia dhamiri mbaya za kihisia zikinishtaki kutokana na namna nilivyowapitisha watoto wangu kutokana na UKIMWI. Yule mwana maombi mwenzangu alinieleza kwamba sijafanya kitu chochote kibaya. Lakini pamoja na hayo kwa miaka mingi niliendelea kujisikia mwenye dhamiri mbaya. Nilikuwa nikijisikia vibaya kutona na ukweli kwamba watoto wangu walifahamu kuwa baba yao alikufa kutokana na UKIMWI. Nilijisikia mwenye dhamiri mbaya kwa sabbu wataishi maisha yao yote huku wakiwa na hofu kwamba ninaweza kufa na UKIMWI wakati wowote. Nilijisikia vibaya kwa sababu mwaka 1998 nilikaribia kufa, na jambo hilo liliwaogopesha sana watoto wangu. Kwa kiwango fulani nililiona jambo hilo kuwa limesababishwa na mimi, yaani kwamba hali ya afya yangu iliwafanya wapitie changamoto hizo. Je, hii ndio sababu iliyowafanya wakawa na matatizo katika maisha yao? Je, hii ndio sababu baadhi yao hawaendi kanisani? Basi unaweza kuona jinsi nilivyokuwa na maswali mengi ambayo nilikuwa nikiwafikiria.

Niliomba ili dhamiri mbaya iondoke; ambao ni mzigo mzito niliokuwa nikiubeba. Kwa sasa siwezi kuyatawala maisha ya watoto wangu. Maana watoto wangu wameshakua na ninahitaji kujisamehe kutokana na dhamiri mbaya iliyokuwa inanisumbua kimakosa. Mimi sikuchagua kupata VVU; sikufanya jambo lolote baya ambalo “limenistahilisha” kupata VVU. Hata kama nilipata VVU kutokana na chaguo baya, basi nilipaswa kujisamehe na kusonga mbele.

Katika 1 Timotheo 1:12-16, Paulo anasema: “Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake; ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani. Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na pendo lililo katika Kristo Yesu. Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi. Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele.”

Hebu tukumbuke kwamba Paulo alikuwa amewatesa Wakristo na alikuwa shahidi wakati wa kifo cha mfia-dini wa kwanza Stefano. Paulo alikuwa ni Farisayo aliyeichukia imani ya Kikristo. Lakini Bwana alimkamata na akayabadilisha maisha yake kwa namna ya ajabu.

Ninajiuliza ikiwa baada ya kuokoka na kuwa mwamini Paulo alijisikia dhamiri mbaya kutokana na familia zilizokuwa zimewapoteza wapendwa wao kutokana na mateso yake. Ninajiuliza kama Paulo alikuwa hapati usingizi kwa kuwafikiria watoto ambao walikuwa wamewapoteza baba zao au mama zao kutokana mateso yake, au ikiwa alijiuliza kwamba hao watoto watakuwa ni Wakristo pamoja na kuwa wazazi wao wameshafariki. Kwa kweli mawazo ya namna hii ni mizigo ambayo ni Yesu tu ndiye anayeweza kuibeba. Huo ndio ujumbe ambao ulinijia tulipokuwa tukiomba pamoja na marafiki waombaji wenzangu. Nilidhamiria na kuamua kwamba sipaswi kubeba dhamiri mbaya kutokana mapungufu yangu, au kutokana na madhaifu yangu, au kutokana changamoto za afya yangu ua makosa yangu.

Kwa mara nyingine niliwaachilia watoto wangu kwa Bwana. Niliachilia dhamiri mbaya kuhusiana na mimi kuwa na UKIMWI. Nililia sana siku hiyo. Kwa kweli nilitamani sana wakati wote kuwapatia watoto wangu maisha mepesi na bora, lakini hali haikuwa kama nilivyokuwa nikitamani. Lakini Yesu alikuja maishani mwetu. Yesu aliyabadili maisha yetu. Yesu ametuwezesha kupita katika yote. Yesu amezisamehe dhambi zetu. Yesu ni Mwamba wetu na Msingi wetu. Ni mara ngapi katika Biblia Mungu amesema hivi: “Sintakuacha wala sintakupungukia?” Ni mara nyingi sana Bwana amesema hivyo.

Baada ya maombi yetu kuhitimishwa, rafiki yangu alinieleza kuwa, “Hebu fikiria kwa namna nyingine. Watoto wako wanaifikiria sana afya yako kwa kuwa wanakupenda. Hiyo pekee ni zawadi tosha. Hebu hilo ndio liwe jambo unalolifikiria sana kuliko kufikiria kwa mtazamo hasi.” Ninapenda na ninapendwa na watoto wangu. Hii ni zawadi ambayo nitaendelea kuifurahia siku zote za maisha yangu.

9

ZABURI YA 119 NA MATESO

Zaburi ya 119 ina aya nyingi sana zinazoelezea juu ya mateso na huzuni. Hebu tuiangalie, mara nyingi shida za kiafya zinatufanya tujizingatie kifikra. Nilipokuwa nimelazwa kutokana na VVU na magonjwa yake nyemelezi, basi hapo nilianza kufikiria juu ya vipaumbele fulani. Na cha kushangaza niligundua kwamba vipaumbele vyangu vilikuwa vimegeuzwa. Sikuwa nimemweka Mungu na familia yangu kama vipaumbele vya msingi. Si kwamba mimi ni mzazi mzembe au mtu asiye amini, bali nilikuwa nashughulikia mambo yanayohitaji uangalizi wa siku kwa siku kuliko mambo yanayoweza kushughulikiwa kwa muda mrefu.

Wakati mwingine huwa ninafikiria kwamba, kwa sehemu Mungu anaruhusu magonjwa ulimwenguni ili tuweze kuvitambua vipaumbele vyetu na ili tuweze kujitoa kikamilifu kwa vipaumbele hivyo ambavyo ni vya muhimu zaidi. Tunaweza kuwa na tabia ya kuvipa thamani sana vitu kama fedha, mafanikio, na mambo mengine kuliko kumfuata Mungu. Tunapokuwa wagonjwa, tunakuwa na wasaa wa kuzungumza na Mungu katika maisha yetu, na hivyo kurudisha uhusiano wetu kwa kumtazama Bwana. Jambo hili linaleta changamoto ambayo inahitaji ujasiri, uvumilivu na kiwango kikubwa cha msaada.

Nilikuwa nikijiuliza mwenyewe, “Je, ni bora niwe na ugonjwa huu ili niweze kujifunza mambo ya thamani au niuruhusu ugonjwa huu uniletee masikitiko na hali ya kukata tamaa?” Basi nikaamua kuutafuta kwanza Ufalme wa Mungu, na huo haukuwa uchaguzi wa mara moja tu. Wakati mwingine

huwa ni uchaguzi unaohitajika kila dakika, au kila saa na hivyo kuufanya uchaguzi huo kutokuwa rahisi.

Ninapoisoma Zaburi ya 119 ninashangazwa na ukweli kwamba mwandishi anasema lilikuwa ni jambo jema kwake kupata mateso ili, "...Nipate kujifunza amri zako" (aya ya 71). Huyu mtunga zaburi aliona kwamba mambo mema yanakuja kutokana na mateso.

Mwaka 1981 nilipojikabidhi kwa Yesu nilikuwa nikifanya kazi kama mtalaamu wa huduma za jamii. Baada ya hapo mchakato wa mabadiliko ulianza, hata hivyo kulikuwa na maeneo fulani katika maisha yangu ambayo hayakubadilika. Na moja ya eneo hilo ni mtazamo binafsi wa kujitosheleza na kujitegemea. Nilikuwa na mkazo mkubwa sana wa kujitegemea mwenyewe kifedha, kimwili, na kisaikolojia, mambo ambayo kimsingi si mambo mabaya, lakini sikupenda kuamini kwamba Mungu anataka kunitunza.

Nilipoteseka kutokana na huzuni na majonzi kutokana na talaka ambayo iliwakumba wazazi wangu nilipokuwa na miaka 14, basi kutokana na simanzi na msongo wa mawazo ulionipata nilisoma sana vitabu vilivyoelezea juu ya namna binafsi ya kujitunza na jinsi ya kuwa na afya ya akili. Nilienda chuoni nikiwa na miaka 17 kwa sababu nilikuwa nataka niishi mimi mwenyewe. Nilihudhuria shule ya wahitimu na kupata elimu katika taaluma yangu ya uhudumu wa jamii na lengo lilikuwa ni ili niweze kujitunza mwenyewe kikamilifu na pia kutoa mchango wangu kwa jamii. Tabia hii ya kujitegemea ilijikita sana katika maisha yangu hata wakati ule nilipompokea Bwana.

Nilipofikia hatua ya kuwa muumini, kwa kweli nilikuwa na ugumu wa kumtumaini Mungu hasa katika ngazi ya maisha ya kimwili, kisaikolojia, na kwa upande wa rasilimali. Nilifikiri kwamba Mungu atanifundisha ukweli wa maisha ya kiroho lakini niliona kuwa hawezi kushughulikia mambo yangu ya kimwili sawa na ambavyo ningeliyashughulikia mimi mwenyewe. Kwa kweli niliona ugumu sana wa kuyaweka maisha yangu chini ya uangalizi wake. Nilikutana na njia-panda ya kimaamuzi kama vile

mtoto anapojifunza kuogelea. Wakati wazazi wanaposimama upande mmoja wa bwawa na kisha wakamwambia mtoto wao aogelee, tendo hilo huwa lina maanisha kuwa mzazi huwa anamwomba mtoto kuyaweka maisha yake yote mikono mwake kikamilifu. Mtoto anapoanza kuogelea, anahitaji kuwa na uhakika kwamba mzazi wake atamshikilia ikiwa ataanza kuzama ili asije kufa-maji. Kiakili nilitambua kwamba Mungu atanitunza lakini niliona ni jambo gumu sana kuyaweka maisha yangu yote mikononi mwake, maana nilihofia asije akaniangusha kama watu wengine walivyoniangusha.

Nilifikia kiwango cha mabadiliko katika fikra zangu na nikaanza kumtumainia Mungu ili aweze kunitunza. Niliweza kufanya hivyo kutokana na ugonjwa usio na tiba, na katika fikra zangu niliona ni yeye tu ndiye wa kumgeukia. Niliyaangalia Maandiko ili nijifunze jinsi ya kuyashinda mashaka, hofu na simanzi. Zaburi ya 119 inasema, “Kama sheria yako isingalikuwa furaha yangu, Hapo ningalipotea katika taabu zangu” (aya ya 92).

Moja kati ya hofu yangu kuu kabisa ilikuwa ni kutokana na ugonjwa wangu, kwamba itafikia siku moja ambapo sintaweza kufanya kazi na hivyo nitaishia kuwa maskini wa kutupwa. Nikiwa mwanadamu niliye na nia ya kujitegemea, kwa kweli umaskini ulikuwa unanitisha sana. Lakini Bwana alilitatua tatizo hili hata kabla sijafahamu kwamba nilikuwa na virusi, yaani kabla hata mume wangu wa zamani hajagundulika kuwa na UKIMWI. Mungu alitangulia mbele yangu na kuiandaa njia.

Kilichotokea ni kwamba mwaka 1987, jirani yetu ambaye alikuwa ni rafiki yetu pia aliingia na kuanza kufanya kazi ya bima. Alitueleza alichokuwa akikifanya katika hiyo kazi yake mpya. Tulimueleza kwamba hatukuwa na bima ya maisha na hivyo tukamwomba ili atuelezee juu ya kazi yake, nilitambua kwamba hatukuwa na bima ya maisha na ikiwa tatizo litatokea kwangu na kwa watoto itakuwa ni shida, lakini Ray alionekana kutolikubali wazo la kuwa na bima ya maisha. Aliamini kwamba tendo la kukata bima ya maisha mara nyingi

lilikuwa linasabibisha kuleta mikosi katika maisha ya mtu. Pengine alikuwa anatabiri juu ya kifo chake mwenyewe, alikataa katakata kuzungumzia juu ya bima ya maisha, urithi, au vitu vyovyote vilivyokuwa vikihusiana na mambo hayo. Kwa muujiza wa Mungu tu, huyo rafiki yetu alipokuja nyumbani na kuanza kutuelezea, Ray alikubali kununua bima ya maisha. Miezi minne baadaye Ray aligundulika kuwa na UKIMWI. Miezi ishirini na mbili baadaye alifariki. Kampuni ya bima ilibidi ichunguze madai yetu maana Ray alikufa chini ya miaka miwili tangu alipojiunga na bima na kwa mujibu wa sera ya bima madai ya jinsi hiyo huwa yanachunguzwa. Lakini tulikuwa hatufahamu kama alikuwa na UKIMWI wakati alipokuwa akisaini bima hiyo na mimi ninaamini kuwa huo ulikuwa ni mpango wa Mungu kwa ajili yangu na watoto wangu. Hilo lilinifundisha kwamba Mungu anafanya kazi katika maisha yangu kwa njia ambazo siwezi kuzitambua hadi baadaye sana.

Tunapotaabika kutokana na ugonjwa mzito unaopelekea mauti, mara nyingi tunakumbana na kiwewe cha kisaikolojia. Hofu ya kuhofia yasiyojulikana inatawala na kuwa na nguvu sana. Lakini Mungu anatusaidia tuweze kuikabidhi mizigo yetu ya hofu kwake. Kwa msaada toka kwa marafiki wenye upendo na toka kwa Roho Mtakatifu, Mungu anakutana nasi tuwapo katika hofu zetu na anatutia nguvu ya kuinuka. Mara nyingi watu huwa wanamwangalia mtu anayeumwa na kusema, “Kwa kweli sijui anawezaje kukabiliana na hali hiyo.” Ninaamini kwamba Bwana ana usaidizi maalumu wa kutoa faraja kwa wanaosumbuliwa na kupitia hali ya kuugua. Hakuna mtu aliye karibu na mwenye kuugua anayeweza kuijua neema ya Mungu maana hiyo ni maalumu kwa wanaoteseka na kutaabika.

Kwa upande wa kimwili, ni rahisi kidogo, maana nafahamu kwamba ninapaswa kunywa dawa, kula chakula kizuri chenye kuleta afya, kufanya mazoezi, na kupumzika. Zaidi ya hayo najiweka mikononi mwa Mungu. “Unitegemeze sawasawa na ahadi yako, nikaishi, Wala

usiniache niyaaibikie matumaini yangu" (aya ya 116). Kila pumzi tunayovuta ni zawadi na ninamshukuru Mungu kwa kila siku mpya anayotupatia. Kitendo cha kulifuata neno la Mungu na kuyakabidhi mahitaji yetu kwa Mungu kinatusaidia sana katika kuondoa msongo wa mawazo, na jambo hilo husaidia kuimarika kwa afya kwa ujumla wake. Ni Mungu tu ndiye anayekifahamu kipindi chetu cha kuishi hapa duniani. "Ee Bwana, rehema zako ni nyingi, Unihuishe sawasawa na hukumu zako" (aya ya 156).

Hatimaye, dhumuni letu kama waamini ni kumpatia Mungu utukufu, maombi yangu na ambayo pia ni maombi ya mtunga zaburi ni, "Nafsi yangu na iishi, ipate kukusifu, Na hukumu zako zinisaidie (aya ya 175).

JARIBU LA KUJINYONGA

Kuna mjadala unaoendela juu ya maadili kuhusiana na kifo cha huruma kwa watu ambao ni wagonjwa sana katika jamii zetu. Wanafalsafa na wana maadili wamekuwa wakihojiana kuhusu uamuzi wa mtu kuchagua muda wa kifo. Wale wanaoamini juu ya haki ya kufa wanaamini kwamba tunapaswa tuwe na uwezo wa kuyasimamisha mateso yetu na maumivu wakati wowote tunapoweza kuamua. Wale wanaopinga wazo hilo wanaamini kwamba Mungu ndiye anayefanya uamuzi kutokana na hekima yake isiyo na mipaka, na kwa wale wanaoumwa, wakati wanapoendelea kutafuta suluhisho la maumivu yao ili kupata faraja, basi wanapaswa pia kukikubali kifo wakati wowote kinapokuja.

Kwa kuwa hali ya kifo ni jambo gumu sana kulizungumzia na marafiki, familia, na watu wengine, basi jambo hili linakuwa gumu sana kwetu sisi ambao tunaishi na VVU/UKIMWI maana hakuna tiba hadi hivi sasa. Marafiki zangu kadhaa wanaoishi na VVU wamejaribu kujinyonga mara kadhaa bila mafanikio kwa sababu hofu ya kuishi na VVU ni nzito kuliko wanavyoweza kuibeba na kuchukuliana nayo. Ingawa sikuwahi kufikia hatua ya kujiua, kuna nyakati hata mimi nilikuwa nikiwaza juu ya kujinyonga. Hata hivyo, kuna sababu kubwa mbili zinazonifanya niendelee kuushikilia uhai nilionao. Kwanza, sheria ya Mungu inatueleza jinsi uhai ulivyo wa thamani na kwamba hatupaswi kuua uhai wowote (ikiwemo uhai wetu wenyewe). Mungu anayo haki ya kuamua idadi ya siku za kuishi kwetu, na hili tunaliona katika Zaburi ya 139 aya ya 16b, “Chuoni mwako ziliandikwa zote pia, Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.” Ujumbe huu ulifikishwa kwangu kutoka kwa mshirika mmoja wa kanisani kwetu aliyekuwa akisumbuliwa sana na ugonjwa wa moyo, na alisema hivi, “Mungu ndiye anayeamua

ikiwa nitavuta pumzi au la, au ikiwa moyo wangu utaendelea kudunda au utasimama."

Kitu cha pili ambacho ninaendelea kukishikilia ni nguvu ya nia ya mwanadamu kuendelea kuishi (nguvu ambayo ninaamini iliumbwa na Mungu). Hata ninapokuwa nimelala katika chumba cha wagonjwa mahututi nikiwa ninaumwa sana, na mwenye udhaifu, na ninayesumbuliwa zaidi ya miaka kumi na mbili iliyopita, mwili wangu uliendelea kupigana ili uweze kuendelea kuishi, na hilo lilifanyika hata wakati mimi nikiwa sina fahamu. Nilipokuwa nimelazwa, niliota ndoto Maninja waovu wakinifukuza katika mwamba, na katika nchi yenye vilima huku wakijaribu kuniua. Nikiwa ndotoni nilikimbia, niliruka sarakasi, nikaruka na kisha kukimbilia mbali, nilikimbia ili kuyaokoa maisha yangu. Kwa upande wangu ndoto hiyo ilikuwa ni mfano unaoonyesha juu ya vita iliyopo katika maisha yangu. Hatimaye nilitafakari juu ya hiyo ndoto kisha nikaona jinsi hisia za mwanadamu zilivyo na nguvu katika kutetea uhai. Kwa sasa siogopi kufa ingawa ninayaogopa mateso na maumivu makali. Ninaamini kwamba baada ya kufa nitaingia katika pumziko la mbinguni. Hata hivyo mwili wangu umeumbwa kung'ang'ania uhai niliopewa.

Kuna wakati tunapopata fikra kwamba tuna uwezo wa kuyatawala maisha yetu. Ndio, tuna uwezo wa kutawala juu ya vyakula tunavyokula, kufanya au kutofanya mazoezi, kuvuta sigara au kunywa pombe, au kujidunga madawa ya kulevya, n.k; lakini zaidi ya hapo sisi ni vyombo tu na fikra hizo zina lengo la kujihakikishia kwamba tupo salama. Yeyote aliyepatwa na tatizo la ghafla kama vile kugundulika kuwa na gonjwa zito sana, au kifo cha ghafla cha mpendwa ambacho hakikutarajiwa, au kuzaliwa kwa mtoto mwenye ulemavu, basi mambo hayo yote yanatukumbusha kwamba hatuna uwezo wowote ule wa kuyatawala maisha yetu.

Kama hatuna uwezo wa kuyatawala maisha yetu, basi mara nyingi huwa tunaona vigumu kuyaweka matumaini yetu kwa Mungu, ambaye ndiye mwenye kutawala, na tunaona vigumu kuupokea mpango wa

Mungu katika maisha yetu. Ninapojifunza kumtumaini Mungu, basi hapo ninaamini juu ya wakati wa Mungu. Mara nyingi huwa ninashangaa na kujiuliza, “Ingelikuwaje kama ningelijinyaonga huku nikifikiria kwamba maisha yangu yamekwisha kabla ya kuwepo kwa dawa za kupunguza makali ya VVU ambazo zimesaidia kuongeza muda wa kuishi kwa watu waishio na VVU/UKIMWI? Kwa kweli ningelikuwa nimeikosa miaka mingi mizuri, ambayo ilikuwa imejawa na baraka nyingi za kifamilia, baraka za marafiki na shughuli za kihuduma. Je, kama kuna tiba itapatikana baadaye ambapo nitakuwa bado ninaishi? Je kama nitakuwa hai ili niweze kuomba na mtu mwingine badala ya kujiua? Ukweli ni kuwa kama ningelijiua, basi bila shaka ningeliyakosa yale ambayo Mungu alikuwa ameniandalia.

Hadi sasa, nimeishi miaka mingi kuliko nilivyokuwa nikitarajia, nimefunga ndoa na mwanamume mwema, nimeshuhudia watoto wangu wakikua na nimewakaribisha wajukuu katika ulimwengu huu. Haya ni mambo ambayo yalionekana kuwa hayawezekani wakati nilipogundulika kuwa na VVU mwaka 1988. Ninatazamia kuwa na uhai zaidi hali nikiwa na matarajio mema na hasa pale ninapoifungua zawadi ya Krismasi.

Kutokana na uzoefu wangu kama mshauri, mara nyingi nilikutana na wateja ambao walikuwa na msongo sana wa mawazo kiasi cha kutamani kujiua. Lakini kusema kweli msongo wa mawazo umebeba udanganyifu, ni kama vile Shetani. Mara nyingi msongo wa mawazo unatueleza kuwa maisha na uhai wake hayana thamani. Yaani ni kama vile tendo la kusafiri safari ndefu ukiwa kwenye treni ipitayo eneo lenye kiza. Tunaweza kufikiri kwamba hatujawahi kuona nuru ya mchana, lakini baada ya safari ndefu huwa tunatokeza upande mwingine wenye mwanga.

Mfadhaiko na msongo wa mawazo ni kitu kinachoendana na sana na VVU/UKIMWI. Bila kujalisha kwamba mfadhaiko huo ni wa kibaiolojia au wa kisaikolojia, ukweli ni kuwa kuna wakati mfadhaiko huo unahitaji uangalizi na wakati mwingine huduma ya

kitaalamu. Watu waishio na VVU wanaojisikia mfadhaiko, wanaojisikia kuwa na hasira za haraka, wanaojiona wenye huzuni sana na wasio na tumaini, au wale wanaopata usingizi kupita kiasi au wasiopata usingizi basi wanapaswa kuonana na madaktari au kuonana na washauri nasaha. Mara nyingi nuru hupatikana baada ya mfadhaiko huo.

Kwa kuwa nina uzoefu wa mambo mengi mema katika maisha yangu, na kwa kuwa nimeshuhudia miujiza mikubwa na midogo, basi ninaliweka tumaini langu kwa Mungu ili aweze kunipatia wasaa aliouandaa kwa ajili yangu, na wala si hali ya kutopata wasaa.

11

MSAMAHA WAREJEWA

Katika sura ya 5, niliandika jinsi nilivyokuwa nikihangaika kumsamehe mume wangu wa zamani kutokana na usaliti wake na kwa kuniambukiza VVU. Nilieleza namna nilivyoweza kuufikia msamaha kama sehemu ya utii kwa Bwana na kama mapito muhimu katika safari yangu. Katika andiko hili, nitatumia vielelezo vya kibiblia juu ya ugumu wa mchakato wa kusamehe na njia nyingi kuelekea msamaha. Zaburi ya 55 imekuwa ya muhimu sana kwa upande wangu katika safari hii ya msamaha.

Kama mshauri wa Kikristo niliyaona mahangaiko ya watu waliokuwa wamejeruhiwa kihisia kama mimi, na wengine ambao walikuwa wamejeruhiwa zaidi kwa namna nyingine. Mara nyingi huwa tunaelezwa, “Samehe na sahau,” msemo ambao unaweza kutafsiriwa kuwa ni, “Hebu shika na uliachilie na ubaki nalo mwenyewe,” na hii ni kwa sababu mara nyingi huwa hatuna ruhusu ya kuongelea maumivu na hasira zetu kwa watu wengine.

Wakati mwingine tunafikiria kwamba msamaha unapaswa kuwa ni jambo la kutolewa kwa haraka—yaani kwamba tunasamehe halafu yanakuwa yamekwisha. Uzoefu wangu binafsi umenifundisha kwmaba mchakato wa kusamehe ni mchakato mrefu na wenye kuchosha, na kwa kweli nimeipata mifano mizuri sana ya kibiblia toka kwa Daudi wakati alipojaribu kulitimiza jukumu hilohilo la kusamehe katika Zaburi ya 55. Katika Biblia iitwayo *“Life Application Bible, Toleo la Nne,”* iliyochapishwa na Tyndale na Zondervan (Toleo la 1991), kuna rejea inayosema kwamba Zaburi ya 55 iliandikwa wakati wa kipindi cha uasi wa Absalum na wakati wa usaliti wa Ahitofeli. Kutokana na chanzo hiki, baadhi ya wanazuoni wa kibiblia pia wanainukuu zaburi hii kuwa imebeba ujumbe wa kimasihi

(aya ya 12-14) ambazo zinaeleza juu ya tendo la Yuda la kumsaliti Kristo. (Rejea 55:1kk, ukurasa wa 962). Tunaweza kuona kwamba usaliti uliowakumba Yesu na Daudi uliwafanya wawe na uamuzi mgumu wa kumsamehe adui aliyekuwa amewaumiza kwa kina, na ambaye kwa wakati fulani alikuwa ni rafiki mpendwa. Maneno ya Zaburi hii, kwa upande mwingine yanaonyesha juu ya uzoefu wetu wa kukutana na usaliti na safari ya kuelekea msamaha.

Mchakato wa msamaha katika Zaburi ya 55 unaanza kwa maombi na Daudi anamwomba Mungu ili amsaidie. Daudi alifahamu kama tunavyofahamu kwamba tuna uhuru wa kwenda mbele ya Baba yetu wa Mbinguni hali tukiwa na maombi na tukiyaweka mahitaji yetu kwake. Daudi anaandika hivi, “Ee Mungu, uisikilize sala yangu, Wala usijifiche nikuombapo rehema. Unisikilize na kunijibu…” (aya ya 1-2a). Kisha akaendelea kuyaeleza maumivu yake makubwa, kwa uhuru kabisa na pasipo hofu ya kuhofia mawazo yake. “Unisikilize na kunijibu, Nimetanga-tanga nikilalama na kuugua. Kwa sababu ya sauti ya adui, Kwa sababu ya dhuluma yake yule mwovu. Kwa maana wananitupia uovu, Na kwa ghadhabu wananiudhi. Moyo wangu unaumia ndani yangu, Na hofu za mauti zimeniangukia. Hofu na tetemeko limenijia, Na hofu kubwa imenifunikiza” (aya ya 2-5). Daudi hakuwa na sababu ya kuzificha hisia zake wala hakuona sababu ya kuzifanya hisia zake ziondoke kiroho. Daudi alikuwa huru kabisa kumshirikisha Mungu Baba yake shida zake, Baba aliye Abba. Hivyo maisha yake yanatuonyesha kwamba mwanzo kabisa katika msamaha ni kuelezea yale yote yaliyo ndani yetu, na tunapaswa kufanya hivyo bila kujali jinsi tendo hilo lilivyo la kuumiza.

Kisha Daudi anarukia katika fikra nyingine ambazo zina lengo la kukwepa mambo, na hata sisi hutenda hivyo mara nyingi, huku tukitamani walau mambo yangekuwa tofauti na yalivyo wakati huo. Mara nyingi tunapojiona kuwa tupo kwenye mtego na tumesalitiwa, basi huwa tunaanza tabia ya kubuni mambo sisi wenyewe. Mara nyingi huwa ninafikiria hivi, “kama jambo hili lisingelitoka, au kama ningelikuwa

nimefanya uchaguzi mwingine, n.k." Inaonekana aina hii ya fikra ipo kwa wanadamu wengi. Wakati mwingine tunaweza kutamani muujiza utokee ili tuweze kukimbia mbali na matatizo yanayotusibu, ili tuweze kuwa huru mbali na maumizi yaliyopo. Kwa kweli ndoto za jinsi hii hazina msaada wowote maana hatuwezi kuurudisha wakati na wala hatuwezi kuyakimbia matatizo yetu, lakini utaona kuwa hata Daudi kwa sababu ya ubinadamu wake alitaka kuyakimbia matatizo yake. Daudi aliandika hivi, "Nikasema, Ningekuwa na mbawa kama njiwa, Ningerukia mbali na kustarehe. Ningekwenda zangu mbali, Ningetua jangwani. Ningefanya haraka kuzikimbia Dhoruba na tufani" (aya ya 6-8). Baada ya kuwa tumejaribu kukwepa kwa kutumia vyakula, luninga, pombe, kazi, au michepuko mingine ndipo hatimaye huwa tunakubali kukabiliana na kile kilicho mbele yetu. Ni jambo la kawaida kutamani kuondokana na hali ngumu au kuondokana na hali yenye kuleta maumivu, lakini kama tunataka kuwa na afya ya kiroho, kiakili, na kihisia, basi ni vizuri sana kutembea na Bwana wakati wa tatizo lolote lile.

Hata pale tunapokuwa tukitaka kusamehe na tunapotarajia kusamehe, kwa kweli bado tunaweza kukabiliana na hisia kali za uchungu. Tunaweza tusiwe na upendo wala kumfurahia mtu ambaye ametusaliti. Na hiyo ni hali ya kawaida ya tabia ya mwanadamu, lakini bado hatupaswi kuiendekeza tabia hiyo kwa muda mrefu maana ina madhara. Tunaweza kushughulikia hali ya kuachilia kwa muda mrefu kidogo ili uchungu uweze kutoka lakini Mungu anafahamu mapungufu yetu na ugumu tulio nao katika jambo hilo. Hebu angalia jinsi Daudi anavyomuuliza Mungu kuwaadhibu watu wabaya! "Ee Bwana, uwaangamize, uzichafue ndimi zao, Maana nimeona dhuluma na fitina katika mji (aya ya 9).

Wakati Daudi alipokuwa akiendelea kukabiliana changamoto za kihisia kutokana na kusalitiwa, inaonekana kuwa alidumisha mawasiliano yake na Bwana. Aliziweka changamoto hizo zote mbele ya Bwana kwa ujasiri mkubwa.

Kama vile kuongezea matusi kwa mtu aliyejeruhiwa, Daudi alikuwa na maumivu ya ziada ya kuumizwa na mtu aliyekuwa karibu yake. Ni jambo gumu sana kuumizwa na kudhalilishwa, lakini udhalilishaji unapotoka kwa rafiki, kwa kweli maumivu yake yanakuwa makali kiasi cha kufika kwenye mifupa. Wakati mume wangu aliponisaliti, kwa kweli iliniuma sana kuliko kama ambavyo ingelikuwa ni kwa mtu mwingine ambaye si mtu wangu wa karibu. Ilionekana kuwa ni jambo lisilofikirika kwa mtu aliyekuwa akidai kunipenda kuweza kuniletea madhara kama hayo. Daudi na Yesu watakuwa walifahamu hivyo pia. Daudi alilia, “Kwa maana aliyetukana si adui; Kama ndivyo, ningevumilia. Aliyejitukuza juu yangu siye anichukiaye; Kama ndivyo, ningejificha asinione. Bali ni wewe, mtu mwenzangu, Rafiki yangu, niliyejuana nawe sana (aya ya 12-13). Inaonekana kuwa Daudi alikuwa akikabiliana na hali ya kutoamini kilichokuwa kikitokea kwamba rafiki anaweza kumtendea vile. Wengi wetu tumekuwa pia tukipambana na hali hiyo!

Daudi anasafiri mbali zaidi na kuweza kutoa msamaha baada ya kuwa amejielezea vizuri kutokana na hasara aliyokuwa ameipata. Lakini kabla hajafikia hatua ya kupata amani, anakutana na hisia zenye chuki zaidi. Daudi anaanza kueleza matamanio yake ya kulipa kisasi dhidi ya maadui zake. Kwa mara nyingine anaonekana kufahamu jinsi isivyokubalika kuleta mawazo mabaya yasiyokubalika mbele za Mungu. Daudi anaamini kwamba hatimaye Mungu atamwongoza katika njia ya haki.

Daudi anatamani kuwafuatilia kwa nyuma Absalum na Ahitofeli huku akisema, “Mauti na iwapate kwa ghafula, Na washuke kuzimu wangali hai, Maana uovu u makaoni mwao na katikati yao” (aya ya I5). Baada ya kukitamka kisasi alichokuwa anakitamani kwa Bwana ili kupata faraja, basi anaomba tena ili Mungu aweze kumwokoa na chuki hizo. “Nami nitamwita Mungu, Na Bwana ataniokoa” (aya ya I6). Ninafahamu kwamba nina mawazo ya kulipiza kisasi kwa watu ambao wameniumiza na ninatamani kuwaona wakiumia na wao. Kwa kweli sifurahii mawazo haya na

hivyo ninamwomba Bwana aubadilishe moyo wangu kila ninapoanza kufikiria hivyo. Mimi ni mtu ninayeamini kuwa kisasi ni cha Bwana na kwamba Yeye ni Mungu wa Haki anayeipima haki yake kwa rehema kwetu sisi wote wenye dhambi.

Baada ya kuwa Daudi amepitia maelezo haya yote ya kihisia, ambayo yanaonyesha jinsi alivyokuwa amejeruhiwa, basi hatimaye anaanza kuitafuta amani kwa kutoa msamaha. Ninaamni kwamba tunakuwa katika nafsi nzuri ya kuweza kumsamehe mtu baada ya kuwa tumeshazieleza kwa kina zile hisia kwa mtu mwingine. Na hapo ndipo tunapoweza kulishughulikia kabisa suala la msamaha. Daudi anakubali msamaha wa Mungu kwake mwenyewe. “Ameiokoa nafsi yangu iwe salama, asinikaribie mtu, Maana walioshindana nami walikuwa wengi” (aya ya I8). Daudi anatafakri juu ya upendo wa Mungu kwake usio na masharti.

Baada ya Daudi kuwa ameumaliza mchakato wa kuachilia ili yatoke na kwenda mbali unaona wazi kuwa ni kama vile Daudi anapumzika na kupumua kwa ahueni. Daudi anasema, “Umtwike Bwana mzigo wako naye atakutegemeza, Hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele” (aya ya 22). Kwa kweli kauli hii imejawa na amani ya kutosha!

Baada ya Daudi kupitia fikra za kutaka mambo fulani yatokee, na baada ya kupitia fikra zenye hasira, huzuni, uchungu, na nia ya kutaka kulipa kisasi, Daudi hatimaye anapata pumziko. Zaburi inaishia kwa maelezo ya ukamilifu na yenye kutoa suluhisho. Daudi anamweleza Mungu wake kuwa, “Bali mimi nitakutumaini Wewe” (aya ya 23b). Mimi pia kama ilivyokuwa kwa Daudi, nimeona kuwa baada ya kusafiri safari ya maumivu, huku nikijieleza vya kutosha kuhusiana na hisia zangu na Mungu Baba yangu mwenye huruma na kwa marafiki wenye kuelewa, basi hapo huweza kufikia kwenye msamaha. Hii ni njia ambayo sisi sote tunaweza kuipitia kwa msaada wa Bwana.

2

MAMBO YA UPENDO

HAPO ZAMANI

Nililelewa pamoja na dada zangu wengine wanne na kulikuwa na hadithi zenye upendo mwingi zikihusishwa na hadithi za Disney—ambapo mtoto wa mfalme na binti wa mfalme walipendana, wakavishinda vikwazo vilivyokuwa vikiwazuia ili wasiwe pamoja na kuishi maisha ya furaha, huku ndege wakiimba, na huku panya wadogo wakilishona gauni la harusi na hatimaye wakawashinda wale waliokuwa wakitaka kuwatenganisha. Kwa bahati mabaya fikra za namna hii hazikuwa fikra zenye uhalisia, si tu kwa kuwa ilikuwa ni hadithi ya kubuni, bali ni kutokana na ukweli kuwa ilikuwa imeacha jambo moja muhimu sana ambalo ni Mungu.

Tunapokuwa nje ya Mungu, tunaweza kuwa na mipango na ndoto zote, lakini mipango hiyo yote na ndoto hizo zinaweza kuvurugika baada ya muda mfupi, na hii haiwezi kamwe kulinganishwa na amani, upendo, na kuridhika kunakopatikana katika mapenzi ya Mungu. Nimeishi kwa namna zote mbili, na nimeshuhudia matokeo yaliyo tofauti sana katika maisha yangu.

Kwa sasa ninaamini kwamba Mungu ni wa muhimu sana katika mchakato wa kuumba, kujenga na katika kuiimarisha ndoa nzuri yenye upendo. Kwa bahati mbaya, sikuweza kulitambua hili katika ndoa yangu ya kwanza na Ray.

Mimi na Ray tulikutana tukiwa chuoni na wakati huo nilikuwa siishi maisha ya kiroho. Nilikuwa nimehudhuria kanisa nikiwa mtoto mdogo lakini niliacha kwenda kanisani nikiwa kigoli na nilikuwa sijampokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yangu. Sikuwa nimetengeneza mfumo wa maisha, na wala sikuwa na imani ya kila siku yenye mahusiano na Bwana. Jambo

baya kabisa ni kwamba mimi na Ray hatukumfanya Bwana kuwa msingi katika maisha yetu. Jitihada zangu zote za kutaka kuwa na ndoa nzuri zilivurugikia mbali. Tuliendelea kuishi tukiwa na wigo uliokuwa umetutenga na alionekana kujijengea wigo zaidi, na hali hiyo ilijitokeza sana miaka michache kabla ya kifo chake. Bila shaka dhamiri ilikuwa ikimshtaki kutokana na kutokuwa mwaminifu, huku akiwa na upinzani fulani kwangu, na pengine alikuwa na mawazo mengine mengi ambayo sikuyafahamu.

Wakati alipokufa nilichanganyikiwa kwa sababu mbalimbali. Jambo ninalotaka kulizingatia hapa ni kule kupoteza ndoto ya kuwa na ndoa nzuri yenye mafanikio. Kwa kweli hiyo ilikuwa ni ndoto yangu kwa muda mrefu na kwa kweli sikushuhudia ndoa ya jinsi hiyo tukiwa na Ray. Kisha nilipogundulika kuwa na VVU, niliamini kwamba sintaweza kuja kuolewa tena na kwamba ndoto ya kuwa na ndoa nzuri yenye upendo haitaweza kamwe kutimizwa. Ingawa niliamini kwamba Bwana anatupatia tamaa za mioyo yetu, kwa kweli niliona kuwa nia yangu hii haiwezi kutimizwa. Kuna aya moja toka katika Maandiko ambayo ilinisimamia vizuri na inatoka katika Zaburi 37:4, “Nawe utajifurahisha kwa Bwana, Naye atakupa haja za moyo wako.”

Aya hiyo iliniongoza kuelekea katika sala zilizo na mafumbo mengi hasa baada ya kifo cha Ray. Kwa upande mmoja, nilitamani kuipata ndoa iliyo na watu wenye kupendana, lakini kwa upande mwingine, niliamini kuwa haiwezekani na nilitamani sana Bwana ayabadilishe matamanio yangu ya kutaka kuolewa na anisaidie niweze kukubaliana na hali ya kuishi kama mseja maisha yangu yote yaliyosalia. Niliomba ili Mungu aiondoe nia ya kutaka kuolewa na aniwezeshe kukubaliana na useja ambao ndio ulionekana kuwa ni njia rahisi katika maisha yangu ya wakati huo. Ni Mungu tu katika hekima yake kuu ndiye angaliweza kutatua mahitaji yangu yaliyokuwa yamechanganyikana na mawazo na hisia nzito na hatimaye akanipatia

namna aliyoona inanifaa. Katika ndoa yangu ya kwanza sikuwa nimetafuta uongozi wa Mungu, hivyo nilijifunza kwanza kuwa ni muhimu kuutafuta kwanza mwongozo wa Mungu, na hii haijalishi hali ya kimaisha itakayokuwepo. Hilo lilikuwa ni fundisho kubwa sana ambalo Bwana alilifunua kwangu kwa namna mbalimbali ambapo niliweza kuuona na kuutambua baadaye uhusiano wa Mungu wenye miujiza na upendo.

Kama nilivyoandika hapo kwanza, kwa kweli nilifanya kazi kubwa sana ya kuweza kumsamehe Ray na hivyo kuweza kuponywa toka katika hasira na uchungu. Ninaamini kwamba hatuwezi kuwa huru kupenda tena hadi pale suala la uponyaji likamilike, au walau mpaka zoezi hilo limekaribia kukamilika, na hadi muda fulani uwe umepita. Nilitambua kwamba nilipaswa kuing'oa mizizi ya uchungu na kutoruhusu isiuharibu na kuuzinga moyo wangu. Nilipokutana na Galen, nilikuwa katika mchakato huu wa uponyaji.

KWA SASA

Mimi na Galen tulikutana Kanisani mwaka 1990. Tulikuwa ni wazazi tuliokuwa tukisumbuka na kuwalea watoto peke yetu. Yeye alikuwa ni mwanachuo aliyehitimu katika lugha ya Kihispania na mimi nilikuwa ni mshauri. Tulikutana tukiwa chini ya faragha ya wazazi walio peke yao na tulifurahia kukutana lakini hatukuendeleza zaidi mahusiano yetu. Sisi sote tulikuwa na shughuli nyingi za kuzifanya pale Kanisani hivyo tulionana mara kwa mara katika shughuli za kikanisa. Basi tuliendelea kuonana mara kwa mara kwa ajili ya chakula cha jioni na kwa ajili ya kunywa kahawa. Na katika tukio moja, mchungaji wetu na mke wake walimwalika Galen na mimi ili twende nyumbani kwao kwa chakula cha jioni. Baadaye tulitambua walikuwa wakijaribu kuwa washenga wapatanishi kati yetu. Mimi na Galen tulikuwa na mambo yanayofanana sana; sisi sote tulimpenda Bwana, tulipenda Kihispania, na pia tulikuwa na imani na miiko inayofanana sana kuhusiana na maisha. Watoto wetu walikuwa marafiki na kuna nyakati tulitoka

kama familia kwenda kutembea tukiwa na wafamilia wengine wa Kanisani. Nikaanza kujisikia kumpenda Galen lakini sikupenda kuendeleza hilo kwa sababu ya mimi kuwa VVU.

Baada ya kuwa tumefahamiana kwa muda wa takribani mwaka mmoja alinipigia simu akiwa na tatizo kubwa. Alinieleza kuwa binti yangu ameeleza katika darasa la Shule ya Jumapili kuwa baba yake amefariki kwa UKIMWI. Alitaka kufahamu ikiwa kulikuwa na ukweli katika maelezo hayo. Nilimweleza kuwa ni kweli na alionekana kuumizwa sana na mzigo ambao mimi na watoto wangu tulikuwa tumeubeba. Nilifikiri kwamba kuanzia hapo ataacha kuwa karibu na mimi kwa sababu kukataliwa ni suala la kawaida kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Hata hivyo, Galen aliendelea kuwa na urafiki na kutuonyesha wema. Nilipata faraja sana kuona kuwa hakunikataa kuwa rafiki yake kiasi kwamba wazo langu la upendo wa kina kwake nikawa nimeliweka mbali. Niliamini kwamba hakutakuwa na nafasi ya yeye kunipenda kimapenzi lakini nilifurahi kwa kuwa alinipokea kama rafiki wa kawaida. Baadaye nilitambua kwamba baada ya kutambua kuwa nilikuwa na VVU alionekana kuhuzunika sana maana alipenda kuwa na mahusiano ya kina na mimi, na hivyo taarifa kuhusu afya yangu zilimfanya aone kuwa uhusiano alioutaka hautawezekana

Wakati mimi na Galen tulipokuwa tukiendelea na safari yetu ya uponyaji, tuliendelea kuonana kanisani na tulikuwa tukikutana kama familia. Niliufurahia sana urafiki wetu na nikawa wazi sana kwake.

Mwaka 1993, mambo yakaanza kubadilika katika uhusiano wetu. Galen alikuwa akijielimisha kuhusiana na VVU, alikuwa ameongea na daktari wake, wazazi wake, na mchungaji wetu na alikuwa akiomba. Alifikia maamuzi kwamba hapendi kunipoteza, na kwamba kwa uangalifu uhusiano wa kina na mtu aliye VVU unawezekana bila kuleta madhara kwa afya yake. Ilionekana ni kana kwamba Bwana anaingilia kwa njia ya kimiujiza na kumpatia Galen upendo wa kunipenda mimi ambapo kwa maelezo ya kibinadamu upendo

huo ulikuwa hauwezekani. Mimi pia niliendelea kumpenda, lakini sikupenda kumwingiza katika hali ambayo ingemfanya asiwe na amani au hali yenye kumhatarisha. Tuliishia kupendana na katika hali ya kushangaza tuliungwa mkono na mchungaji wetu, tuliungwa mkono na familia zetu na tuliungwa mkono na kanisa na watoto wetu. Ninaamini hilo lilitokea kwa mapenzi ya Mungu na kwa kweli limekuwa ni jambo jema sana kwetu sisi sote. Mwaka 1994 tulifunga ndoa chini ya mchungaji yule yule na tangu wakati huo nimebarikiwa sana kwa kuwa na mume mwema na mwenye upendo. Kwa kweli Bwana ni sehemu ya ndoa yetu. Wakati wote tunaiweka ndoa yetu, maisha yetu, watoto wetu, shughuli zetu, na magumu yetu yote mbele za Bwana. Tunashirikishana matumaini yetu na ndoto zetu, tunashirikishana pia ushindi na kushindwa kwetu mbele za Bwana.

Kwa kweli ninashindwa kufikiria namna nilivyopata kuwa na mshirika mwenye upendo kama huyo. Upendo wake ni mkuu sana kwangu na upendo wake ulionekana kwangu wakati nilipougua sana. Alisimama pamoja na mimi katika ugonjwa huu wa mauti, na alisimama na mimi katika changamoto ya kuwatunza vijana watano, na alisimama na mimi katika milima na mabonde yote ya maisha pamoja na changamoto za kiimani tulizozipitia.

Kwa upande wangu, upendo wa Galen ninaulinganisha na upendo wa Yesu Kristo. Yesu ananiona mimi kuwa ni rafiki yake mpendwa, na wala hanioni kama ni mtu niliyepotoka. Yesu hanitazami kama mtu "niliyeathirika na UKIMWI" na wala hawaoni wana wake kama "walevi" au kama "bidhaa zilizoharibika," au "wenye dhambi?, au kama .....(jaza mwenyewe). Wakati Yesu anaponiangalia, na kwa kuwa nimeokolewa kwa neema yake kwa imani, basi ananiona mimi kuwa ni msafi nisiye na doa wala mawaa yoyote yale. Haniangalii na kuuona "UKIMWI." Hawatazami wafuasi wake kuwa wasiopendwa kwa namna yoyote ile. Upendo wake hauna masharti. Yesu anapowaangalia wana wake anaona uzuri na ukamilifu kwa kuwa tunavipata hivyo kupitia haki yake.

Galen ananiangalia mimi kwa namna iyo hiyo. Upendo wake ni kama upendo wa Kristo. Galen hanifanyi nijisikie kuwa ni mdhaifu au mwenye mapungufu kwa sababu ya UKIMWI. Ananipenda kama nilivyo. Kwa kweli sijawahi kukutana na upendo kama huo katika maisha yangu. Kwa kweli Mungu amenipatia matamanio ya moyo wangu kupitia kwa mpendwa wangu Galen.

NYONGEZA KWA TOLEO LA MWAKA 2010:

Biblia inasema, “wala kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi” (Mhubiri 4:12). Mimi na Galen tunamtegema Yesu ili kutufanya tuwe na “uzi wa tatu” katika ndoa yetu. Katika ndoa yetu mara nyingi tunatafuta mwongozo wa Mungu na tunamwalika ili awepo katika uhusiano wetu.

Hivi sasa ninapoandika, mimi na Galen tumeishi kwa miaka kumi na sita yenye baraka katika ndoa yetu, ni miaka mingi kuliko wengi wetu walivyokuwa wamefikiria. Upendo wetu umekuwa imara na wa kina katika miaka tuliyopitia na kwa kweli bado ninamshangaa sana Mungu kwa kunipatia Galen kuwa mshirika mwenza. “Mi amado Galeno” ni zawadi ya Mungu kwangu na ni mfano wa upendo wa Mungu wa kina kwangu.

ZABURI YA 118

Mwaka 1998, miaka kumia tangu nilipogundulika kuwa na VVU, niliugua sana nikalazwa nikiwa na tatizo la ugonjwa uitwao kwa lugha ya kitabibu *pancreatitis*, ambao ni ugonjwa hatari wa kuvimba kongosho. Sikuwa nimetambua hapo awali kwamba nilikuwa pia nimeanza kupata ugonjwa mwingine uitwao kwa kitaalamu *sepsis* na hivyo nikajikuta nikiwekwa katika chumba cha wagonjwa mahututi kwa siku kadhaa. Nilipewa dawa za kunilaza usingizi ili nisiweze kutoa sindano ya kuingizia maji kwa njia ya dripu za kawaida. Maana madaktari walikuwa wakitumia sindano hizo kunipatia dawa za kuua wadudu na dawa nyingine. Pia niliugua homa ya mapafu, homa kali, na maambukizi mengine. Pia kiwango cha VVU mwilini kiliongezeka sana kufikia 700,000 na seli za T zinajulikanazo kitaalamu kama *T-cells* zilishuka na kufikia kwenye 100, na ndizo zilizosababisha niwe na homa hizo zote kutokana na UKIMWI. Katika hali hiyo nilikuwa nimevuka kutoka kwenye VVU kwenda kwenye UKIMWI.

Baadaye nilipatwa na tatizo la mishipa ya moyo na kwa sababu hiyo madaktari waliwaita wanafamilia yangu kuja hospitalini kwa kuwa waliamini kwamba nitakufa na kwamba sintaweza kufika asubuhi yake. Magonjwa yote niliyotaja hapo juu ukijumlisha na UKIMWI vingeliweza kuniua, sembuse na kupata tatizo la moyo juu yake, kwa sababu moyo wangu ulisimama kwa dakika nne. Lakini kwa kupitia rehema za Mungu nilihuishwa toka mauti. Mimi ninaamini kuwa huo ulikuwa ni muujiza, na nilipozungumza na daktari kuhusiana na hali niliyokuwa nayo alisema kwamba niliweza kuwa hai kwa muujiza tu, na alisema huo ulikuwa ni muujiza KABLA ya kujumlisha shambulio la mishipa ya moyo!

Kwa kweli nilishangazwa sana na hali niliyoipitia. Kwa kweli niliona kwamba kwa kupitia muujiza wake Bwana aliamua kuyalinda maisha yangu. Baadhi ya watu walio na mashaka wanaweza kusema kwamba madaktari waliokoa maisha yangu, mimi pia ninaamini kuwa walifanya hivyo, lakini ninaamini kwamba nilikuwa ninaumwa sana kiasi kwamba madaktari pekee wasingeliweza pasipo Mungu kuingilia kati.

Nilipopata fahamu na kufahamu kilichotokea, nilishangaa sana kuona Mungu amenipata nafasi nyingine ya kuishi. Nilikuwa na maswali mengi sana—kwa nini Mungu alinihifadhi? Alinihifadhi kwa dhumuni gani? Nitautumiaje muda uliobakia niliopewa? Nitawezaje kukabiliana na zawadi hii kubwa niliyopewa? Kwa kweli nilichanganyikiwa na hivyo nikajikuta nakuwa mnyenyekevu mbele za Mungu. Nilishukuru sana kwamba nimeokolewa, lakini niliona kuwa sikuwa ninastahili kile ambacho Bwana amenipatia.

Maswali mengi niliyokuwa nayo yalinifanya niingie katika maombi mengi sana nikitaka majibu ya maswali yale. Kwa kweli majibu yalikuwa yapo wazi. Moja kati ya majibu hayo ni kwamba nilikuwa nimepewa muda zaidi wa kuweza kuwa pamoja na Galen, na familia yangu, na marafiki zangu. Na kweli hilo pekee lilikuwa ni jibu ambalo mtu analihitaji, lakini bado niliona kwamba kuna mengi sana ya kufanya. Ninaamini kwamba wakati Bwana anapoingilia na kutenda miujiza ni lazima kuna madhumuni yake. Ninakumbuka katika Agano la Kale jinsi Mungu Baba alivyofanya, na jinsi Yesu alivyoingilia na kuyasimamisha magonjwa, upofu, ulemavu, na majanga mengine ya kiasili. Na inaonekana kwamba miujiza hiyo ilifanywa kwa madhumuni.

Kwa mfano, Mungu alileta mapigo ili kumshawishi Farao aweze kuwaachilia Wayahudi toka Misri. Yesu aliwaponya wagonjwa ili kuuonyesha uungu wake na kuthibitisha kwamba alikuwa ni Masihi. Pia aliwaponya watu ili kuziimarisha imani zao. Miujiza ya jinsi hiyo ni kama vile Yesu alivyomfanya Petro kutembea juu ya maji.

Petro alitembea juu ya maji lakini alianza kuzama na akalia, “Bwana, niokoe.” Kisha Yesu akamshika mkono akamwambia, “Ewe mwenye imani haba...kwa nini uliona shaka?” Wakati huo imani ya Petro iliimarika na akasema, “Hakika wewe ni Mwana wa Mungu” (Mathayo 14:28-32).

Baada ya kifo cha Kristo na kufufuka kwake, Petro alimponya kiwete aliyekuwa ombaomba kisha akaongea na watu waliokuwa wamekusanyika pale. Moja kati ya dhumuni lake la kumponya yule ombaomba ilikuwa ni kuwafundisha watu waliokuwepo kuhusu Yesu. Petro alisema, “Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote” (Matendo ya Mitume 3:16). Mifano hii ya kibiblia imenionyesha kwamba Mungu anaponya kwa madhumuni maalum na kwamba dhumuni hilo ni kutuelekeza kwenda kwa Mungu.

Sasa, sikupata uponyaji dhidi ya VVU. Nilikuwa na bado nimeathirika na VVU. Hata hivyo, niliponywa kutokana na magonjwa mengine yaliyokuwa yakiyatishia maisha yangu.

Nilipokuwa nikiomba na kutafakari juu ya maswali yangu ya kwanini nilitambua kwamba kulikuwa na dhumuni kuhusiana na uponyaji wangu. Nilifikiri kwamba pengine Bwana alitaka nifanye aina fulani ya shughuli za kihuduma. Hata hivyo, katika hali ya udhaifu wangu sikuweza kutembea, je ningeliwezaje basi kufanya shughuli kadhaa za kihuduma? Basi niliona kwamba ninachoweza kukifanya ni kuomba zaidi na nilitumia muda mwingi kwenye maombi. Pia nilitumia muda fulani kuzijenga nguvu zangu za kimwili na kurudisha afya ya mwili. Niliamua kujiunga na kushiriki kikamilifu katika kikundi cha usaidizi cha VVU kilichokuwepo kanisani kwetu na nilimwomba Bwana anionyeshe ninachopaswa kukifanya.

Kadri nilivyoendelea kutafuta huduma ya kufanya, siku moja niliona kuwa nimelipata jibu nilipokuwa nikishiriki mafunzo ya Biblia. Jibu lilikuwa

ni rahisi sana kiasi nilitamani kujicheka kwa kuwa nilikuwa sijalifahamu hapo kabla. Siku hiyo nilipitia Zaburi ya 118 na katika ile aya ya 17 nilishangaa sana. Aya hiyo inasema, “Sitakufa bali nitaishi, Nami nitayasimulia matendo ya Bwana.” Kwa kweli maelezo niliyoyapata katika aya hii yalinipa uzoefu wa kushangaza kiasi cha kusema “Ahaaa!” Maana aya hii ilikuwa rahisi na ilieleza bayana na hivyo ikanipatia majibu kwa maswali yangu yote niliyokuwa nayo hapo kabla. Tunaponywa ili tuweze kuwasimulia wengine juu ya upendo, rehema, neema, na huruma za Mungu wetu.

MTANDAO WA DUNIA NZIMA

Katika sura iliyotangulia nimeandika juu ya ugonjwa wa kudhoofisha niliougua mwaka 1998 nikiwa na ugonjwa unaoathiri kongosho ujulikanao kwa kitalaamu kama *pancreatitis,* na huku nikiwa na magonjwa mengine yaliyoniandama wakati huo kama vile ugonjwa wa *sepsis,* UKIMWI, shida katika njia ya hewa, homa kali, pamoja na maambukizi mengine. Kwa kweli ulikuwa ni wakati wenye maumivu sana kimwili na kihisia kwangu mimi na kwa familia yangu. Nilikuwa sina uwezo wa kujipa msaada na hivyo niliwategemea watu wengine kwa mahitaji yangu yote, na kwa kweli nilishangazwa sana na upendo na matunzo tuliyopokea wakati huo.

Nilipougua, Galen wangu alituma haraka sana maombi ya kuombewa kwa marafiki zetu wote na kwa wana familia wetu wote. Kwa kweli tulipokea upendo mkubwa sana na maombi ambayo yalitoka karibu sehemu zote za nchi yetu. Marafiki zetu waliwaeleza marafiki zao wengine kutuombea, wanafamilia waliwaeleza wanafamilia wengine kutuombea kiasi kukawa na mtandao wa maombi, kwa kweli tulikuwa hatujawahi kuona maombi ya kimtandao kama hayo katika maisha yetu. Kwa kweli lilikuwa ni jambo la kushangaza, la kuvutia, na lenye kutia moyo. Ndugu zetu walisafiri kwa ndege toka California, Washington, na Carolina Kaskazini ili kuja kuwatunza watoto wetu. Kwa kweli nilikuwa sijawahi kupata ugonjwa mzito kama huo hapo kabla na hivyo sikuwahi kuwa katika uhitaji mkubwa kama ilivyokuwa wakati huo, ni hadi pale nilipolazwa ndipo nilipoona uhitaji wa jinsi hiyo.

Washirika wa Kanisani kwetu walimpatia Galen na watoto wetu vyakula vilivyopikwa kwa zaidi ya wiki

tano, na walikuwa wakileta mara tatu kwa wiki. Tulipokea kadi nyingi na barua zenye ujumbe wa kututia moyo na zenye kutupatia uhakika kwamba walikuwa wakituombea.

Afya yangu ilipoimarika huku nikirudiwa na fahamu na kuweza kufahamu kilichokuwa kimetokea, nilitambua bayana kwamba kama yasingelikuwa maombi na usaidizi toka kwa wapendwa na kwa msaada wa Bwana, ni hakika kuwa nisingelikuwa hai hadi wakati huo. Kwa kweli nilipotambua hivyo nilipatwa na furaha sana. Niliona kuwa Mungu aliamua kutenda kazi kupitia kwa mtandao wa waombaji ambao ulikuwa hauonekani kwa macho, lakini mtandao huo ulikuwa ni imara kama vile chuma.

Familia yetu ilikuwa haina msaada na ikakumbatiwa katika upendo wa Yesu ulioonyeshwa na wapendwa mbalimbali. Kwa kweli sijawahi kuupata upendo mzito toka kwa wapendwa na kwa Bwana kama wakati huo. Kwa kweli upendo huo uliniacha nikiwa mtu niliyebadilika kabisa. Ulinifanya nijinyenyekeze zaidi maana nilishangaa sana kuupata upendo kama ule.

Niliweka nadhiri ya kwamba na mimi nitakuwa na upendo kwa watu wengine, hata kama haitalingana na upendo nilioonyeshwa na wapendwa. Mungu hakuzizuia nyakati zenye maumivu kutufikia, lakini kupitia nyakati hizo Mungu alitufundisha mambo ambayo yamekuwa ni hazina kubwa kwetu.

UGONJWA WA LAZARO

Mazingira ya kiutamaduni kuhusiana na VVU/UKIMWI hapa Marekani yamepitia mabadiliko mengi sana katika historia ya ugonjwa huu. Kilichoonekana hapo awali kuwa ni “Ugonjwa wa Mwanamume Shoga” ulienea haraka sana kwa watu ambao si mashoga yaani wenye mahusiano ya kawaida ya kimapenzi. Wananchi watu wazima pamoja na vijana wote wapo katika hatari ya kuupata ugonjwa huu. Badiliko jingine lililotokea ni mabadiliko toka “kufa kwa UKIMWI” na kuwa “kuishi na UKIMWI.” Badiliko hili lilikuja kutokana na ujio wa dawa mpya za kuongeza muda wa kuishi kwa kupunguza makali ya VVU, maana dawa hizi zina uwezo wa kuzuia kuzaliana kwa virusi, na kwa sababu hiyo mtu aliye na VVU anaweza kuishi muda mrefu akiwa na kinga thabiti mwilini mwake. Ingawa dawa hizi zimesaidia katika kuongeza umri wa kuishi kwetu sisi tulio na UKIMWI, ukweli ni kuwa bado si tiba kamili ambayo tunaihitaji.

Kabla ya ujio wa dawa hizi, matarajio ya muda wa kuishi kwa mtu aliyekuwa na “UKIMWI uliokomaa” ilikuwa ni mwaka mmoja au miaka miwili tu. Watu wengi waliofikia hatua hii ya ugonjwa kabla ya ujio wa tiba hizi mpya waliambiwa kuweka mambo yao sawa, yaani walipaswa kuandaa maelezo ya urithi, kuweka fedha katika mashirika ya bima, kuwatembelea ndugu, na kisha kujiandaa kwa ajili ya kifo. Katika hali ya kushangaza wengi kati ya wale waliokuwa wameambiwa kujiandaa na kifo waliendelea kuishi kwa muda mrefu kiasi cha kufikia hatua ya kuzitumia dawa hizi mpya zenye mchanganyiko na wakaanza kujisikia vizuri zaidi na hivyo kuzishinda nguvu za kirusi. Jambo la kushangaza katika uandishi mwingi unaohusiana na VVU, msemo unaotumika kuzungumzia maandalizi hayo ya kifo na kisha kukutana

na “ufufuo” wa wazi, msemo huo huitwa “Ugonjwa wa Lazaro.”

Maelezo haya yananukuuu hadithi moja ya kibiblia ambapo Yesu alimfufua mtu aliyekufa na akawa hai. Yesu aliionyesha huruma yake kwa mtu huyo na kwa familia yake waliokuwa wakiteseka kutokana na kumpoteza ndugu yao. Ingawa jamii ya watu waishio na VVU haijamgeukia Bwana kwa idadi kubwa, bado waliamua kutumia msemo wa kibiblia katika kipindi hiki kingine cha kuishi na UKIMWI. Je, kuna mwangaza wa Mungu uliojaa neema na rehema uliohusika katika kuvumbua na kutengeneza dawa hizi mpya ambazo zimepunguza kwa kasi kiwango cha vifo na kuwahurusu watu wengi kuishi muda mrefu zaidi? Ni Mungu tu ndiye anayeweza kulijibu swali hili lakini ni wazi kuwa rehema zake haziwezi kutuangusha kamwe.

Katika maisha yangu nimepitia Ugonwa wa Lazaro mara mbili. Mara ya kwanza ni wakati nilipoanza kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU, dawa ambazo nilipaswa kuzitumia zikiwa na muunganiko wa dawa tatu. Kabla ya wakati huo kulikuwa na dawa ya aina moja iliyokuwa ikitumika na kwa kweli haikuweza kuzuia kuenea na kuzaliana kwa virusi. Mwaka 1996, mfumo wangu wa kinga ulianza kudhoofika na kushindwa kufanya kazi na hapo ndipo nilipoanza kutumia dawa mpya. Pasipo dawa hizo ni hakika kuwa ningeliingia katika hatua ya UKIMWI mapema. Kutokana na uwepo wa dawa hizo niliweza kufanya kazi hadi ilipofikia mwaka 1997. Nilianza kuamini kwamba pengine nina muda fulani wa kuishi na nikawa na imani kwamba ninaweza kuishi kwa muda hadi pale tiba itakapopatikana. Hivyo, niliupitia Ugonjwa wa Lazaro kwa namna ya kuwa na matumaini, si tumaini tu kutokana na dawa za kisasa, bali tumaini kwa Bwana. Bwana anafahamu idadi ya siku zangu hapa duniani, na hivyo ninaamini kwamba siwezi kuishi siku nyingi au siku chache kinyume na Mungu alivyonipangia. Pia ninajifunza kwamba Yeye aliyeuumba ulimwengu ananitunza na mimi kwa namna binafsi. Kwa

kweli siwezi kulielewa na kulielezea vizuri hili wazo! Kwa upande wangu, tumaini husaidia katika kuishi maisha yenye matarajio mema kuliko kuishi na mfadhaiko na hali ya kukata tamaa. Kwa kweli Mungu ndiye mwenye kukiinua kichwa changu.

Uzoefu wangu wa pili kuhusiana na Ugonwa wa Lazaro ulinijia mwaka 1998, nimekwisha elezea juu ya kilichotokea wakati huu, ni kipindi kile nilichougua sana na kukaribia kufa. Ninaamini Bwana aliingilia kwa neema yake kuyahifadhi maisha yangu. Hivyo, kwa sababu mbalimbali alizo nazo Mungu muda wangu wa kuishi hapa duniani ulikuwa haujaisha.

Hatimaye nilifikia hitimisho kwamba kwa kuwa Mungu amenipatia muda wa ziada ya kuishi na kwa namna yenye muujiza, basi maisha yangu yote yaliyosalia yalikuwa yamehifadhiwa. Uhai wangu ulikuwa ni “zawadi itolewayo bure.” Na kwa sababu hiyo nimeyakabidhi maisha yangu yote yaliyosalia kwa Mungu. Hapo zamani nilikuwa nikifikiria kuwa uhai na maisha yangu ni “mali yangu,” lakini nilipotambua juu ya upendo wa mkono wake uliokuwa umenifikia, basi nilijifunza kwamba ni muhimu kukabidhisha maisha yangu kwa Mungu na kisha kumtumainia Yeye na kumruhusu atende anavyoona vyema kwangu. Bwana anatushikilia kama vile kuku anavyowakumbatia vifaranga wake.

Nilirejea katika hali ya uzima karibu kabisa na majira ya Ufufuo (Pasaka) siku ya kusherehekea mika 45 tangu kuzaliwa kwangu.

16

ZAWADI YANGU

Zawadi yangu imenifanya niweze kufika mbele ya kiti cha enzi cha Mungu aliye mkuu.

Zawadi yangu imenipatia furaha isiyo na kifani kwa kuwa nimeweza kuwaangalia wengine wanaonizunguka kwa ujasiri.

Zawadi yangu imenifanya nisafiri safari ya kiroho na kihisia na hivyo kunisafisha uchafu wa vumbi na tando za buibui zilizokuwa ndani yangu.

Zawadi yangu imenipatia ujasiri wa kuwaonea wengine huruma hasa wale waliovunjia moyo.

Zawadi yangu imenionyesha nguvu kuu na uweza wa Mungu.

Zawadi yangu imeniruhusu kuiona miujiza mingi sana.

Zawadi yangu imenifanya niwe na tumaini lililo karibu na linalomtumainia Mungu.

Zawadi yangu imenifanya nipokee uamsho wa nguvu za upendo usio na masharti.

Zawadi yangu imenipitisha na kunivusha katika bonde la uvuli wa mauti.

Zawadi yangu imenifanya niwe mnyenyekevu.

Zawadi yangu imenigeuza kichwa changu na kunifanya nisiwe nisiye na matunda.

Zawadi yangu imenipatia fursa ya kuushangaa wema wa Mungu.

Zawadi yangu imenipatia nafasi nyingine.

Zawadi yangu imenipatia upendo toka kwa mtu wa kimungu, ambaye ni mtu sahihi.

Zawadi yangu imenifanya niweze kukua.

Zawadi yangu imenimiminia upendo wa watu wengi, wanafamilia na marafiki.

Zawadi yangu imenifundisha kwamba mwili huu wa nje ni sehemu ndogo sana ya jinsi nilivyo.

Zawadi yangu imenionyesha kwamba ni Bwana tu ndiye anayezijua siku zetu, hata kama ni muda mrefu au mfupi.

Zawadi yangu imenitia moyo wa kuweza kuwafikia wengine.

Zawadi yangu imenitoa katika eneo langu la starehe ili niweze kusema na kuandika ujumbe huu.

Zawadi yangu imenigeuza vipaumbele vyangu.

Zawadi yangu imeonyesha wazi kwamba Bwana wangu ni mume kwa wajane na baba wa wasio na baba.

Zawadi yangu imenijaza sifa na kicho cha kumwabudu Baba yangu wa Mbinguni.

Zawadi yangu imeufanya moyo wangu uwe laini na wenye kukunjika.

Zawadi yangu imenishangaza kwa shukrani nyingi sana.

Zawadi yangu imenifundisha kuikubali na kuishukuru kila siku niliyopewa na Mungu.

Pamoja na mambo yote ambayo zawadi yangu imenipatia, ni wazi kuwa ningeliiacha zawadi yangu kama ningeweza, unajua zawadi yangu ni VVU.

17

MANENO YA ZIADA

Tangu niliposikia maneno ya kuhuzunisha kuwa "Una VVU" maisha yangu yamebadilika sana. Nilipaswa kuachana na nadharia potofu ya kujitegemea binafsi na badala yake nikaanza kumtegemea Mungu. Kwa kweli Mungu ni mwenye rehema sana! Kwa sababu amenipitisha na kunivusha katika dhoruba na maumivu ya kihisia, katika ugonjwa wa kufisha, na katika majanga ya kiroho. Mungu ameniruhusu kuwa na maisha mapya ambapo ninatamani zaidi kuendelea kuishi kwa kuzifuata njia zake kuliko kuzifuata njia zangu. Pamoja na changamoto nilizonazo bado ninayafurahia maisha kwa kuwa Mungu ni mwema na ananibariki. Mungu ni baba mwenye upendo na mwenye kututunza na ambaye hawezi kutuangusha.

TOLEO LA NNE LA MWAKA 2010

Nilipokuwa nikikichapa kitabu cha Kivulini Mwa Yesu mwaka 2001, kwa kweli nilikuwa sifikirii kabisa ninaweza kufikia wakati wa kuwa nimekaa katika kompyuta yangu mwaka 2010, huku nikiwa nimeshaishi miaka ishirini na mbili tangu nilipogundulika kuwa na VVU; na hali nikiwa na afya njema na nikiwa namfurahia Bwana na huku nikiendelea kujifunza masomo yaliyomo katika kitabu hiki. Mimi ni mtu ninayejifunza kwa taratibu sana. Bado nina UKIMWI lakini bado Mungu anaendelea kufanya kazi ya uponyaji katika maisha yangu, na ninaendelea kuomba ili kupata uponyaji halisi. Kwa kweli Mungu amekuwa mwema sana kwangu.

Mathayo 7:7 inasema, "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa." Ninajifunza kwamba Mungu anataka asikie maombi ya

mioyo yetu kwa kadri tunavyoendelea kuishi katika huduma, katika unyenyekevu, na katika upendo. Nimekuwa jasiri katika kuomba na Mungu ameyasikia maombi yangu.

Mwaka 1998 niliona kwamba ninaweza kufa baada ya miaka michache tu, niliona kana kwamba sintaweza kuwaona watoto wangu wakikua na kuwa watu wazima. Niliendelea kuomba ili niweze kuwaona watoto wangu wakihitimu maana kuanzia hapo wangeliweza kujisimamia wenyewe. Kwa neema yake Bwana alinipatia kile nilichokuwa nimekiomba. Nilifurahi sana kuwaona watoto wangu wakihitimu. Baadaye nilipata ujasiri wa kumwomba Mungu ili anipe nafasi ya kuwaona watoto wangu wakihitumu elimu ya chuo kikuu. Mwaka 2004 nilikuwepo wakati watoto wangu wote walipokuwa wakihitimu masomo yao ya chuo kikuu. Baadhi ya watu wanaweza kufikiri kwamba sina shukrani lakini mimi niliuchukulia mstari wa Biblia wa Mathayo 7:7 kwa umakini wake wote na ninaamini Bwana anataka kutupatia mema. Mathayo 7:11 “Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?” Nikiwa kama mama nilitaka kufanya kile ambacho kitawanufaisha watoto wangu, lakini Mungu Baba yetu anatupenda zaidi na anataka kutubariki zaidi.

Hali nikiwa na uelewa huo akilini, niliomba ili niweze kuona watoto wangu wakifunga ndoa. Nilifikiri kamba ikiwa watakuwa wamefunga ndoa, basi watakuwa wamepata mwenzi wa kuweza kusaidiana nao katika maisha yao. (Ninajua kuwa wananagu walikuwa hawafikiri hivyo bali hivyo ndivyo akina mama tunavyofikiria). Nilifurahi sana kuhudhuria ndoa za watoto wangu. Nilimfurahia sana Mungu kwa kunipatia muda mrefu wa kuishi na kuweza kusherehekea katika fursa hizo muhimu. Kisha nikaendelea kuomba ili Mungu anisaidie niweze kuwaona wajukuu zangu. Kwa neema ya Mungu aliniwezesha kuwaona wajukuu zangu. Tarehe 9 Agosti 2010 tulimpokea mtoto aliyepewa jina la Reeci Belle hapa ulimwenguni. Mungu ni MWEMA sana!